Ufunuo, Kitabu Cha Mifano

Habari za asuhuhi, marafiki. Ni hivyo vibaridishi vilivyokuwa vikinitatiza.

Kwa hiyo tuna furaha kuwa hapa asubuhi ya leo kwa muda mchache tu, ku—kuongea na ninyi. Nami sidhani Ndugu Neville ana mahali fulani po pote katika Maandiko ambapo atapachukua kwa ajili ya shule ya Jumapili, kwa hiyo sisi tutaninii tu, labda tumwache tu Roho Mtakatifu, kama tunavyojisikia kuongozwa ku—kuanzia na po pote Yeye anapotaka, ama sura ipi tutakayosoma. Kwa namna fulani nalipenda jambo hilo kwa jinsi hiyo, hakuna kawaida ya sikuzote basi, hakuna utaratibu wa kawaida, tunalipokea tu jinsi lilivyo kutoka kwa Bwana, na kuendelea moja kwa moja.

2 Nami nimekuwa na shughuli nyingi sana. Tulikuwa na mkutano mzuri sana kwenye Maskani ya Cadle. Na sehemu yake iliyo nzuri sana, mbali na kuponya, kwa maoni yangu, ilikuwa ni usiku wa jana, ule mwito wa madhabahuni, ambapo mamia walitiririka kwenye mstari kule, na kujaza nafasi yote kwenye madhabahu, na kila marefu ya kanisa, na huku na huku pande zote, nao walikuwa ni watu waliokuwa wanamjia Bwana Yesu Kristo. Na hilo ndilo jambo muhimu, hata hivyo, ni kuona watu wakizaliwa mara ya pili, wakija Mbele za Mungu.

3 Na kuona kundi hili dogo hapa, hatuna madhehebu yo yote, wala uanachama. Tuna ushirika tu mmoja kwa mwingine. Wale wanaokuja, sisi tunawahubiria Injili.

4 Nilitaka tu kuwatambuliza asubuhi ya leo, ndugu wawili kule nyuma ninaowajua vizuri sana, marafiki wangu wawili wasiri. Ndugu Sothmann, kutoka Canada, yeye na rafiki yake. Wao wametoka kule, naamini wao wana-. . .Yule mtu wa peremende, unaishi wapi, ndugu? Siwezi. . .Halafu ndugu aliye karibu nawe pale. Iowa, sawa. Anakula peremende yake, akishuka kuja barabarani; ilinipasa kujua alipoishi, sivyo? Kwa hiyo tuna furaha sana kuwa pamoja nao leo, kama marafiki wetu wanaotutembelea. Wao wanajitayarisha, nafikiri, kwenda Canada sasa.

5 Kisha turudi kwenye mkutano unaofuata utakaokuwa kwenye, kuanzia juma hili, sehemu ya mwisho ya juma hili, na tarehe ishirini na tatu, huko Minneapolis, Wafanyi Biashara Wakristo.

6 Alhamisi usiku, tutakuwa Chicago, kwenye Chicago Gospel Tab-. . .Ninaamini ni Kanisa la Philadelphia, naam, Alhamisi, usiku wa Alhamisi hii ijayo huko Chicago.

7 Alasiri ya leo, tulipaswa kuwa kwenye Junior Cash mnamo saa nane, nami nilifikiria, kama kila kitu kikienda vizuri, kwa

ajili ya kuwekwa wakfu kwa maskani hiyo. Na—nafikiri yeye alisema alikuwa na bubu wachache. Kwamba, neno limeenea juu ya kuponywa kwa yule bubu kule Indianapolis, ambaye alizaliwa bubu, naye alikuwa na umri wa kama miaka ishirini na minane, naye hajawahi kuongea wala kusikia. Nao wanawaleta mabubu wachache alasiri ya leo. Laiti ningaliingilia jambo hilo sasa na kuwaombea. Na hiyo ni kwenye moja ya kale. . . hii ya 3 ya kale, Barabara ya 3 ya Taifa, juu kidogo tu ya Charlestown. Iwapo ninaweza kufika kule.

8 Nina mambo mazito mengi sana yanayonibidi niyakimbilie nikayafanye sasa hivi. Na kwa hiyo basi kesho, kule chini, sina budi kushika safari kwenda Kentucky. Na kwa namna fulani ninakuwa na shughuli nyingi sana. Lakini baada ya kuimaliza mikutano hii sasa, nina wakati mdogo, nina likizo ndogo. Nitarudi kwenye majuma sita. Ninaenda Canada na halafu kule Pwani ya Magharibi. Kwa hiyo iweni katika maombi kwa ajili yangu, nina maamuzi mengi sana ninayopaswa kufanya mara moja, maamuzi muhimu sana, kwa hiyo niombeeni. Nitakuwa nikiwategemea ninyi kuniombea.

9 Sasa ibada usiku wa leo, kama mchungaji wetu mpenzi, Ndugu Neville, ambaye daima amekuwa wa kutia moyo. Na kuja asubuhi, nilifikiria ningekuja tu, niketi, nimsikilize akizungumza. Bali yeye ni mtu mmoja aliye na heshima sana, kwamba yeye anataka tu mtu fulani. . . Yeye "anapendelea." Nafikiri hayo ni Maandiko, "kupendeleana mmoja kwa mwingine," mnaona. Na—napenda jambo hilo. Nami nina hakika sote tuna furaha kwa ajili ya Ndugu Neville, mchungaji wetu, akiwa mtu wa namna hiyo. Mtu alivyo, ndivyo alivyo moyoni mwake. Mnaona? Hivyo, naye akijionyesha namna hiyo, inaonyesha alivyo yeye.

10 Sasa mimi kwa namna fulani nimekuwa ninii. . . Vema, kwa kweli, nimesimama yapata dakika thelathini na tano, kwa hiyo ninatatizwa hapa nianzie wapi. Nina mahali patatu palipotolewa hapa kwenye Maandiko. Nimeandika mahali pamoja kutoka Petro wa Kwanza, na hapo pengine kwenye Kitabu cha Yuda, na pengine kwenye Ufunuo. Sasa tutaanzia wapi zamu hii? Bwana na atusaidie sasa, na atubariki sana na baraka nyingi, tunapomwangalia Yeye.

11 Kwa hiyo, natumaini ya kwamba vibaridishi havitamkatia mtu ye yote upepo mwingi sana. Vinafanya hivyo? Ama, nafikiri hiyo zaidi sana ni kwa ajili ya mimbarani. Sivyo, Ndugu Cox, *hiki* hapa? Naam, vema, bila shaka ninashukuru. Ki—kinanidhuru sana, hiki bila kifuniko juu ya kichwa changu. Naomba. . . Wanawake wanapaswa kuwa na kifuniko kule juu; lakini si, nadhania, wanaume hawapaswi. Ziling'oka, na vinyweleo havikufunika kule nyuma, mahali nywele zilipong'oka; na upepo ulio mdogo kabisa, nami ninapwelea

katika dakika chache. Kwa hiyo, kwa namna fulani inanibidi kuangalia jambo hilo. Uzee unakufanyia jambo fulani, sivyo?

12 Loo, lakini, hebu tujaribu Kitabu cha . . . Ninahofu nitaingia kindani sana kama nikijaribu kuingia katika Kitabu cha Yuda hapa, kwa maana kiko kwenye "maasi ya Kora," na, "kulifuata kosa la Balaamu, na kuangamia katika maasi ya Kora," jambo ambalo labda litatuchukua muda mrefu. Tunataka kuwaombea wagonjwa walio hapa asubuhi ya leo.

13 Hebu tufungue Ufunuo, na tuanzie hapo kwa aya moja ama mbili, tupate msingi mdogo na kufundisha kwa dakika chache, mpaka watoto watakapotoka. Nasi tutafunga na kuwaombea wagonjwa, mara moja. Sasa, Kitabu hicho ndicho Kitabu cha mwisho cha Biblia. Na hakuna mtu hapa ndani . . . Kitabu kiki hiki kilisema:

> Ya kwamba *hapakuwa na mtu mbinguni* ama *juu ya nchi* ama upande wa chini wa *nchi* aliyestahili ama *aliyeweza* kukichukua *hicho kitabu*, kukifungua, wala kuzifungua zile muhuri, wala cho chote kile.

Hakuna mtu, askofu mkuu, ama ye yote yule; yeye "hastahili," wala hakuna njia ya kufanya jambo hilo.

> Ndipo Mwana-Kondoo akaja, aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, *akakitwaa kile kitabu katika mkono wa kuume wake yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi*, na, kwa kuwa alistahili, naye akakifungua na kuzifungua zile muhuri.

14 Kwa hiyo hebu tu tumwombe kama Yeye atatufungulia Hilo asubuhi ya leo, na kulifunua, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

15 Baba yetu wa Mbinguni, leo tunakushukuru Wewe kwa ajili ya majaliwa ya kuja Kwako kwa njia ya maombi, na kwa kuamini na kuwa na imani ya kwamba Wewe utatimiza lo lote tunaloomba. Kwa sababu, si kwa sababu ni sisi tunaoomba, bali kwa sababu tunatii ulilosema Wewe, "Ombeni; mtapokea. Hamna, kwa kuwa hamwombi. Hamwombi, kwa maana hamwamini." Na, Baba, tunapenda kukuomba Wewe, kwa sababu tunaamini ya kwamba tutapokea tuliyoomba.

Na jambo la kwanza, Baba, kwa ajili ya dhambi zangu mwenyewe pamoja na dhambi za kusanyiko hili, asubuhi ya leo, naomba kwa unyenyekevu msamaha wa dhambi zote za kutokutii, na dhambi za kukosa kufanya, na zo zote zile. Tunaomba, Mungu, ya kwamba utaisafisha mioyo yetu na nafsi zetu, sasa hivi, kutokana na uovu wote, dhambi zote, makosa. Na hebu Roho Mtakatifu afanye upya ndani yetu moyo wa kweli na nia, kukutumikia Wewe. Tujalie, Baba.

Pia tunaomba ya kwamba utawaponya wagonjwa wote na wanaoteseka, na kwa Neno. "Imani chanzo chake ni kusikia,

na kusikia Neno la Mungu." Naomba sasa Roho Mtakatifu aingie na—na kulichukua Neno, aliingize moja kwa moja kwenye mioyo hiyo mipya na misafi iliyo kule, na alipande na imani kuu ambayo itawapeleka juu zaidi, juu zaidi barabarani, hata wamefika Mbele za Bwana Yesu na kupokea kuponywa kwao, baraka wanazoomba. Kwa kuwa, jambo hilo ndilo lililotuleta, ni kukuomba Wewe, na kusali, na kusafishwa na kusuguliwa sana, na—na kuponywa, na kurudishwa katika utumishi tena, Bwana, kukutumikia katika kila kona ambalo Wewe umetutuma. Tunaomba haya katika Jina la Bwana Yesu, Mwana wa Mungu. Amina.

16 Kitabu cha Ufunuo kilikuwa ni kutiwa muhuri kwa ushuhuda wa mwisho wa Bwana Yesu. Nacho kilitolewa . . . Sura ya kwanza, tutaanzia hapo. Nilikuwa ninafikiri labda tutaanza kwenye ile mifano mingine. Sasa, Kitabu chote kimeandikwa katika mifano. Ni vigumu kupata kitu cho chote ambacho ni Neno moja kwa moja, ambapo utaliweka moja kwa moja na kusema . . . Ni kwa mifano. Naye Mungu ana njia ya kufanya jambo hilo, na sababu ya kufanya jambo hilo. Mungu hafanyi kitu bila kuwa na sababu ya kukifanya. Na mtu ye yote . . . Hili ni darasa sasa. Hivi mtu ye yote angalifikiria, sababu ya Yeye kufanya jambo hilo? Hii hapa, ili kwamba angeweza, "kuyaficha macho yenye hekima na akili na kuwafunulia watoto wachanga ambao wangejifunza." Hivi si Yeye ni mwema, kutufanyia namna hiyo?

17 Sasa, kama wanachuoni mashuhuri, na kadhalika, walikuwa na Injili yo—yote jinsi walivyoipanga, hatuna budi kukubaliana na jambo hilo, ndipo wangetoka hapa nje na kufanya kila namna ya mapokeo na kadhalika, nasi tungekuwa na wakati mbaya sana. Nao wanalipata kwa kunena katika njia yao ya kielimu, mpaka, mbona, Hilo lingekuwa linapita juu ya vichwa vyetu nasi hata hatungejua kitu juu Yake.

Bali tunashukuru sana ya kwamba Baba yetu mwema wa Mbinguni aliwarehemu maskini na wasio na elimu, kama nilivyo mimi; kuniahidi mimi, mwenyewe; na wewe, ya kwamba kama tungeketi tu chini na kuomba, ya kwamba angejifunua Mwenyewe kwetu. Si hilo ni zuri sana?

Kanuni zetu zote za imani na miamsho yetu, na kila kitu tulicho nacho, hivyo vyote vimeongezwa tu.

18 Kuna jambo moja tu ambalo kila mtu anapaswa kufanya kumjua Kristo, "Mwamini Bwana Yesu kwa moyo wako wote, utaokolewa."

Kwa hiyo sasa tuna namna za mabatizo na tuna kanuni tofauti za imani, na kutofautiana katika mambo tunayofanya, na mambo madogo yaliyopangwa. Bali hayo yote ni ya kujitengenezea. Mahali tu tuliokota jambo *hili* kisha tukafanya hoja ndogo juu yake, na upande *huu* na kufanya hoja ndogo,

Waprebiteri, na Wakiinjilisti, na wa Kimsingi, na kadhalika, na Wapentekoste, na Waholiness, na Wakalvini, nao wote wana nadharia ndogo zinazowaongoza, wanapofanya fundisho kutokana na jambo hilo.

Kwa kweli, jambo tu ni kwamba, "Mwamini Bwana Yesu." "Yachunguze Maandiko, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi," akasema Yesu.

19 Sasa, jinsi lilivyo jambo rahisi, basi, ya kwamba haidhuru jinsi gani—jinsi gani mtu ye yote anavyoweza kuwa *mjinga* (hiyo ni kusema, "asiye na elimu,"), mtu ye yote awezavyo kuwa, wao wanaweza kuwa watakatifu na watauwa kama askofu mkuu. Mnaona? Hilo ni zuri sana? Hata uwe duni namna gani, au wewe—au wewe ni mfalme ama ungeweza kuwa mzurura mitaani, Mungu anakupenda vivyo hivyo, naye alikufa tu kwa ajili ya kahaba kama alivyokufa kwa ajili ya mtawala. Mnaona? Naam. Unaanza kuyafikiria mambo hayo, ndipo ina—inabadilisha kila kitu. Sivyo? Inabadilisha mwelekeo wote wa moyo. Inabadilisha maoni yako kwa Mungu.

20 Wakati mwingine, hapa, kwa kuwa tunaegemea kidogo kwenye kuteuliwa. Na hiyo ndiyo sababu nilibadilisha asubuhi ya leo, kutoka katika Petro, kwa sababu mara chache zilizopita nimekuwa nikigusia sana kuteuliwa, nilifikiri labda niondoke kwenye jambo hilo kwa muda kidogo tu, kwa maana mngefikiri. . . Sitaki kukwamia kwenye jambo lo lote. Lakini, jambo nililokuwa nikiwazia hapa, mtu fulani anasema, "Ndugu Branham, kama Mungu, kuteuliwa, naam, na kama yeye ameita kwa kuteuliwa, vema, basi, jamani, nitafanya tu jambo lo lote nitakalo." Vema, hilo linaonyesha hujateuliwa bado. Naam. Hiyo ni kweli. Mnaona?

21 Kwa sababu, ungempenda Yeye sana, kufikiri ya kwamba—ya kwamba Yeye alikupenda sana wakati ulipokuwa mwovu, na kabla hujakuwa na uhusiano wo wote na jambo hilo, Yeye alikuchagua. Ungewezaje kukataa jambo lo lote kama hilo? Mbona, inaonekana kwangu kana kwamba lingeweka tu, jambo hilo lingeweka kuteuliwa juu sana kuliko—kuliko torati. Lingeiweka, la sivyo lingeweka wazo la kisheria. Mbona, lingepita cho chote kile; kuwazia kwamba, wakati nilipokuwa nisiyependeka, Yeye alinipenda. Na kuwazia, wakati sikuwa na kitu cha kufanya juu yake, Yeye aliniinua akaniokoa, kwa ajili ya neema Yake. Hakika inanipasa kuwa na shukrani kutosha kumtumikia Yeye na kumpenda. Mnaona? Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyojisikia juu yake tunapozihesabu baraka tena.

22 Na wazia, vipi kama Mungu alisema, "Sasa, ni wale tu walio na cheti cha shule ya sekondari, ama wasiopungua digrii mbili za chuoni, wanaoweza kuwa watumishi Wangu."? Vema, sisi watu maskini, wasiojua kusoma, tungefanyaje? Ama, jamani, ninajizungumzia ninaposema, "sisi." Ninamaanisha

"mimi," mimi na jamaa yangu, mnaona. Tungefanyaje? Ye yote wetu angefanyaje? Maskini wake hao wadogo wa nyumbani wangefanyaje? Vipi kama Yeye alisema, "Makasisi tu ndio watakaookolewa, wahudumu tu, hao tu. Hao wengine wote wataninii tu. . . Yeye atatoa tu mfano na kuwafanya hao watu kuishi sawa nusu?"? Ninyi maskini wake wa nyumbani mngefanya nini, nanyi nyote? Mngepotea. Vipi kama Yeye angelisema tu, "Wazungu wataokolewa, hao tu; watu weusi, watu wekundu, watu wa kimanjano, hakuna mmoja wenu aliye na uhusiano wo wote ndani yake, nyote mmepotea"? Hivi jambo hilo halingekuwa baya sana?

23 Nina furaha sana Yeye alisema, "Ye yote atakaye, na aje tu." Hilo, haidhuru, kijana, mzee, mdogo, mweusi, mweupe, mwekundu, cho chote kile, njoo tu, unywe kutoka kwenye chemchemi ya Bwana, bure. Haikubidi kulipia kitu cho chote, hata kidogo. Na, kumbukeni, baada ya mwaliko kutolewa, bado huwezi kuja mpaka akuite na kukuteua. Hiyo ni kweli. "Hakuna mtu awezaye." Hapa Yeye anasema, "Chemchemi ni bure kwa kila mtu, wala hakuna mtu atakayekuja asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Halafu wakati kubisha [Ndugu Branham anagongagonga mimbara—Mh.] kunapofanywa, na kusema, "Ninakualika uje, ule pamoja Nami. Enyi watoto, karibuni!"

24 Ungewezaje kuukataa huo? Hiyo ingeonekana, kwangu mimi, kama kukosa akili, ku—kukataa mwaliko wa namna hiyo, baada ya Baba mwema wa Mbinguni. . . Si kuwa tu na ushirika hapa, bali kuokolewa milele, kuishi pamoja Naye katika wingi wa ninii Yake, wingi wa neema Yake, na katika Wake. Na kubadilisha nia hii ya kale ya kimwili na ile iliyo safi, takatifu, na iliyotakaswa! Na kubadilisha mwili huu wa kale, mnyonge, na unaofifia, na kuubadilisha na usiopatikana na mauti ambao hautashindwa kamwe! Na kupokea taji ambayo itadumu! Na kubadilisha mauti kwa Uzima! Na kubadilisha kuzimu kwa Mbinguni! Kubadilisha huzuni kwa furaha, loo, jamani, na anakuita "njoo"! Ungewezaje kuukataa? Unaona? Ungewezaje kuukataa? Ni—ni jambo la kutisha sana kufikiria lile wazo la kuukataa. Sivyo?

25 Na, lo, jamani, ninapenda kumwona Mungu akiwaponya watoto Wake, bila shaka. Msinielewe vibaya. Lakini sababu moja nimekuwa nikiona, kama ukiona hivi majuzi, nimekuwa nikijaribu, kila mahali niendapo, kama nikipata mwaliko, kujitahidi kuingia kuhubiri kidogo tu. Nimepunguza kuhubiri kwangu, na kutilia uzito sana upako na kushughulikia se—sehemu ya Milele. . . ya mambo ya kimbinguni, hasa, ambapo, wakati, kuona maono. Nayo ni mazuri sana, nami namshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hilo, bali hata hivyo kuhubiri Neno kumepita hilo kwa maili milioni moja, ninapoona viwete wakitembea, na vipofu wakiona.

26 Usiku wa juzi, wakati bibi huyo aliyekuwa ameketi pale, amepooza kwa yabisi hiyo kavu, naye akifa kwenye kiti alichokuwa amekalia. Naye Bwana Yesu, kwa neema Yake, akaonyesha ono juu yake, akamwita kutoka kwenye kiti hicho. Daktari wake alinijia chumbani, na kusema, "Kasisi Branham, nataka kukuuliza, ulifanya nini?"

27 Nikasema, "Hakuna kitu. Ilikuwa ni imani yake katika Bwana Yesu, ndiyo iliyofanya jambo hilo."

28 Sasa sisi sote tunapenda jambo hilo! Na jinsi tunavyolipenda, kuona viziwi na mabubu, waliozaliwa viziwi na bubu, kwenye ulimwengu ambao haujapata kuzungumza wala kusikia, wanaketi tu pale kama kisiki, halafu kumsikia mtu huyo akisimama na kuzungumza na kusikia. Hiyo ni ajabu! Lakini, loo, hakuna kitu kama kuona mtu aliyepotea akija, wakilia wakielekea madhabahuni, wakisema, "Mungu, nirehemu mimi, mwenye dhambi!" Huyo bubu atakufa tena, aliyepooza atakufa, wagonjwa wote watashikwa na ugonjwa tena kisha wafe. Bali nafsi hiyo iliyookolewa, imeokolewa Milele, milele, haitaangamia kamwe. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, anayemwamini Yeye aliyenipeleka, yuna wa milele, Uzima wa Milele; wala hataingia Hukumuni, bali tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Kwa sababu, wao walimwamini Bwana Yesu Kristo. Amina. Hilo ni la ajabu?

29 Loo, hilo linapaswa tu kuanzisha kurejea kwa upendo utakaoenea tu kila mahali ulimwenguni. Hivyo ndivyo Yesu alivyotaka Hilo lifanye, Injili kila mahali ulimwenguni. Inapaswa kuifungamanisha mioyo ya wanadamu hata hawawezi kulala usiku na mchana, mpaka watu wawe wanaokolewa.

30 Mwangalie Paulo, "Mfungwa," yeye alisema, "wa Bwana Yesu," Myahudi aliyetumwa kwa Mataifa. Watu wake walimfukuza mara tu alipowageukia Mataifa. Mnaona? Bali yeye akawa mfungwa wa Bwana Yesu.

31 Kama vile ingekuwa katika Afrika. Mzungu anamdhalilisha sana mtu—mtu mweusi kule, mpaka kama hata ukikutwa unashirikiana, "Loo, jamani, ni jambo la kuchukiza vipi!" Mnaona, wakiwaita kila namna ya majina, hata wao hawaamini watu weusi wana nafsi, wengi wao. Basi kufikiria ya kwamba mzungu basi anaitwa, mtu kama Paulo, aliitwa kwa ajili ya wokovu wa mtu huyo. Namshukuru Mungu jambo hilo haliko Marekani na nchi nyingine nyingi, bali nimekuwa kule. Labda kwa mtu wa kimanjano, "Enendeni kwa wote!" Naye Paulo akasema, "Mimi ni mfungwa wa Bwana Yesu, lakini," akasema, "Ninakikuza cheo changu katika Bwana." Jinsi upendo wa Mungu ulivyomshurutisha kwenda miongoni mwa Mataifa wachafu, waliofikiriwa kwamba ni "mbwa." Lakini Paulo alisema, "Ninakikuza cheo changu katika Bwana, kwa maana amenipa nafasi ya kwenda kuwahudumia 'mbwa,'" hata hivyo.

32 Yesu, Mwenyewe, alimwangalia yule mwanamke Mtaifa, kama tulivyo sisi, sisi watu hapa, mwanamke Msirofoinike, na kusema, "Si vizuri kukitwaa chakula cha watoto na kuwapa mbwa."

33 Yule mwanamke akasema, "Hiyo ni kweli, Bwana, lakini mbwa wanakubali kula makombo yaangukayo kutoka mezani pa Bwana zao."

34 Hilo lilimshika. Hilo lilimwamsha Roho Mtakatifu, akijua ya kwamba hivi karibuni macho ya Wayahudi yatapofushwa, naye alikuwa basi atawageukia Mataifa.

35 Ninataka kuwapa siri ndogo. Bwana amenibariki sana, naye Ndiye ninayemsifu, kwa kuwaombea wagonjwa. Nami nimeangalia jambo hilo katika miaka hii, nami nimeliona kuwa ni kweli kabisa. Siwezi kamwe, kamwe kufaulu kuomba mpaka hasa nimeingia moja kwa moja katika ushirika halisi na mtu yule ninayemwombea. Huna budi kushuka na kuihisi hali na mtu huyo.

36 Hapa si muda mrefu uliopita, kule chini Mexico. Mwanamume mzee maskini wa Kimexico, mtu mweusi, nywele zina mvi, na masharubu yake yenye mvi, kamwe hajakula, labda, chakula kizuri maishani mwake. Naye huyu hapa anakuja jukwaani; kwa imani, ni Mkatoliki; akienda huku na huku, huku amejifunika shali ndogo, hana viatu, miguu yake ina makunyanzi. Alikuwa akinitafuta. Na wakati alipopiga magoti mbele zangu, nilimwinua kwa mkono wangu. Akanyosha mkono kutafuta shanga zake, na ni shanga za zamani zilizochakaa; alikuwa amezisugua sana, kukariri sala yake. Nikasema, "Hilo halifai, baba. Si lazima kufanya jambo hilo. Ziondoshe, kwa muda kidogo tu." Mfasiri akimwambia. Ndipo akapapasapapasa akanipata. Nikasema, "Njoo hapa tu, baba. Ninakutaka umwamini Bwana Yesu." Basi akainua juu mikono yake mizee, akanishika mabegani, akaegemeza kichwa chake kwenye bega langu. Nikaitazama hiyo miguu mizee yenye makunyanzi, yenye mavumbi, michafu. Nikatoa kimoja cha viatu vyangu, nione kama vingemtosha. Ni afadhali ningeenda miguu mitupu kuliko kumwona akitembea namna hiyo. Mnaona, moyo wangu ulimwonea huruma. Alikuwa kipofu.

37 Sasa, hapo ndipo kweli unapozama ndani ya jambo hilo. Utamaduni wetu wote utashindwa. Ishara zetu zote zitashindwa. Karama zetu zote zitashindwa. "Lakini upendo haushindwi." Huo ndio unaoshikilia, kushika kwa nguvu.

38 Nami nikafikiria, "Maskini mzee, yapata umri angalikuwa nao baba yangu, kama angalikuwa anaishi." Ndipo nikawazia, "Labda yeye ana mtoto, pia, mahali fulani." Naye alikuwa anagugumiza jambo fulani, naye mfasiri hakunifasiria. Ndipo nikamwangalia mzee huyo. Nisingalininii tu. . . Si kwa macho yangu, bali moyoni mwangu, ningalininii tu. . . kama matone

ya manjozi yakianguka. "Maskini mzee wa watu!" Nikawazia, "Labda hajawahi kula chakula kizuri maishani mwake; nguo zilizochakaa." Ndipo nikazama pamoja naye, nikazama katika mateso yake. Nikawaza, "Mbali na kuwa maskini, mbali na hali yake na mateso yake, yote hayo, angali katika ulimwengu wenye giza, hawezi kuona, ni kipofu." Nikawaza, "Ee Mungu, vipi kama huyo angalikuwa ni baba yangu anayesimama pale?" Ndipo nikapata hali ana—anavyosikia. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, mrehemu maskini mtu huyu kipofu." Haikuwa kuomba kutoka kichwani mwangu. Ilikuwa ni Kitu fulani moyoni mwangu, kikiombea jambo hilo. Mnaona, ule upendo!

39 Ndipo nikamsikia akitamka, [Ndugu Branham anaigiza lugha ya kienyeji ya mtu huyo—Mh.] Na hapa Wamexico, kwa makumi maelfu, walikuwa wanapiga makelele. Nilishangaa ilikuwa ni nini. Yeye alikuwa anapiga makelele, "Ninaweza kuona! Ninaweza kuona!" Hapo akageuka na kupiga magoti, akaaza kusugua viatu vyangu, akijaribu kunipapasa miguuni. Nami nikamwinua. Naye akakimbia huko na huko, yule mzee aliyepinda mgongo, akipiga makelele, [Ndugu Branham anaigiza huyu mtu akinena katika lugha yake ya kienyeji—Mh.] "Ninaweza kuona! Ninaweza kuona!"

40 Ilikuwa ni nini? Kuingia katika ushirika pamoja naye. Upendo, huo ndio unaofanya jambo hilo. Hakuna kujitahidi; ni upendo tu msafi, usioghoshiwa. Huo utashinda karama zote za kuwekea mikono. Huo utashinda kufasiri kote na kunena kwa lugha. Huo utashinda ninii zote . . . Ningesema, katika sauti nzuri za kuimba. Huo utashinda kila kitu, kama utaingia tu katika upendo wa Mungu pamoja na mtu unayejaribu kumleta kwa Bwana Yesu.

41 "Loo," unasema, "Ndugu Branham, Mimi siwaombei wagonjwa. Nina mtu . . . "

42 Vema, kama yeye hajaokoka! Usijaribu kujifanya. Roho Mtakatifu anajua vema zaidi ya hilo. Usiwe mnafiki. Unamaanisha kweli jambo hilo. Nawe anza kumchunguza maskini rafiki huyo wako aliyepotea, mpaka kwa kweli huwezi kuvumilia jambo hilo, usiku na mchana. Huna budi kuwaendea tu katika upendo. Angalia kile Roho Mtakatifu atakachofanya. Yeye atamvuta moja kwa moja kwako, kila wakati. "Upendo wa Mungu unatushurutisha."

43 Aisee, hata sijaingia kwenye somo, na hapa umefikia wakati wangu wa kufunga; watoto wanaingia. Hebu tusome aya moja, hata hivyo.

Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu . . .

44 Napenda hilo. Nanyi je? "Ufunuo." Ufunuo ni kitu gani? Ni kitu kilichofunuliwa. "Ufunuo wa Yesu Kristo," hivyo ndivyo Biblia hii ilivyo. Biblia hii ni kwa ajili ya kumfunua Yesu Kristo. Mwanzo humfunua Kristo. Kutoka humfunua Kristo.

Loo, jamani! Nikiingia mle ndani, nitakuwa mwana dini mara moja, ama kujisikia namna hiyo. Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, Kumbukumbu la Torati, Yoshua, vyote, kila kitu, hata kwa Naomi, Ruthu, Ayubu, vyote ni ufunuo wa Yesu Kristo, ili kwamba katika Yeye ukae utimilifu unaofunika mahali pote na wakati wote. Na yote ambayo Umilele unashikilia ni Yesu Kristo. Na mambo haya yote madogo hapa ni mbegu tu kwa ajili ya Siku hiyo kuu ya mkutano wakati jamii ya binadamu itakapojulishwa, katika ufufuo, kwa Bwana Yesu. "Ufunuo," Mungu akifunua.

45 Mti humfunua Yesu Kristo. Ua humfunua Yesu Kristo. Maisha yaliyotakaswa humfunua Yesu Kristo. Hakika. Wasema, "Ua lingewezaje kumfunua Yesu Kristo?" Linakufa katika majira ya kupukutika majani na kufufuka katika majira ya kuchanua. Amina. Linatumikia mahali pake duniani, na kupamba. Linafungua moyo wake mdogo namna *hiyo*, na kusema . . . Mpitaji, angalia, "Loo, hilo si ni jambo la ajabu sana! Ni harufu ya namna gani! Ni nukato zuri jinsi gani, kunusia hilo ua!" Naye nyuki anakuja, anasema, "Nitatoa sehemu yangu." Naye mtembezi anakuja na kutoa sehemu yake. Nalo linafanya kazi mchana na usiku, lipate kudumisha mng'ao, kujitoa kwa mtu mwingine. Si ajabu Yesu alisema, "Yatafakarini maua ya mashamba, jinsi yanavyotenda kazi, wala hayasokoti. Na hata hivyo nawaambia, ya kwamba Sulemani, katika fahari yake yote, hakuvikwa namna hiyo."

46 Basi, hilo ua lilikuwa linamfunua Kristo. Yeye aliitwa, "Nyinyoro ya Mabondeni, Ua la Uwandani." Mnaliona?

47 Jinsi bwana nyinyoro, mchungaji nyinyoro, yeye ni shule nzuri sana, ni mwalimu mzuri sana wa Biblia, ndivyo alivyo bwana nyinyoro; yeye huingia mahali penye giza sana, sana, anajisukumiza mwenyewe kwenye giza la duniani. Ili, afanye nini, ajitukuze mwenyewe? Kutukuza kila kitu kinachomkaribia. Naye hana budi kufanya kazi usiku na mchana kusudi adumishe wangavu wa uzuri wake, kufanya manukato yazidi kutiririka. Yeye anavutwa, mchana na usiku, kutoka ardhini, apate kutoa.

48 Hivyo ndivyo Mkristo halisi anavyofanya. Unaomba na kujinyenyekeza, na kudumu mbele ya Mungu, usiku na mchana, ili kwamba upate kujitoa kwa mtu mwingine. Si kile unachoweka, ni kile unachotoa, ndicho muhimu. Huna budi kujitoa kwa wengine. Hivyo ndivyo Yesu alivyofanya, Yeye alijitoa kwa wengine.

49 Na Ufunuo huu Wake hapa, Ufunuo wa mwisho ulioandikwa!

> *Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo hayana budi kuwako upesi; . . .*

50 Hiki ndicho Kitabu cha Mwisho, Naye alimtuma malaika Wake kushuhudia jambo Hilo.

> . . . *akatuma* kushuhudia *kwa mkono wa malaika zake akamwonyesha mtumwa wake Yohana;*

51 Jamani, jinsi tungeweza siku. . . kudumu hapo kwa juma moja. Angalieni, Hicho ni Ufunuo, ndivyo kilivyo Kitabu hiki, kwa "watumwa" wa Mungu kwa ajili ya wakati wa mwisho, "wakati wakati umewadia," wakati Kitabu hiki kitakapofunuliwa. Sasa, ndani ya Kitabu hiki, tunaona ya kwamba Kitabu hiki kilikuwa kimefungwa, na kufungwa kabisa, na kutiwa muhuri, mpaka wakati wa mwisho. Kote kote katika nyakati wao wamejaribu jambo hilo. Kumbukeni, Biblia ambayo ilitolewa kutoka katika mkono wa Mungu aliyeketi kwenye Kiti Chake cha Enzi, ilikuwa imefungwa, na kutiwa muhuri kwa muhuri saba upande wa nyuma, na hakuna mtu Mbinguni na duniani, mahali po pote, aliyestahili kukitwaa kile Kitabu, wala kufungua muhuri zake, wala hata kuangalia mle. Bali Mwana-Kondoo alikuja akakifungua.

52 Mnamkumbuka Danieli? Danieli, kwenye mwisho wa wakati, yeye aliona, ono lake la mwisho, mwishoni mwa huduma yake; mwenye kuona maono.

53 Basi angalia hapa, "akamtuma malaika Wake," yapata miaka sitini na kitu baada ya Pentekoste, Huyu hapa "akimtuma malaika Wake kushuhudia mambo ambayo hayana budi kuwako upesi."

54 Sasa, Kitabu cha Ufunuo kilipata kuandikwa lini? Kwanza, kiliandikwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Na, Yohana, kwa moyo uliojazwa Roho Mtakatifu! Mnaona?

55 Viumbe vya kimalaika hushirikiana pamoja. Loo, natumaini mtapata jambo hilo, hilo limeshuka chini moja kwa moja, bure. Angalieni! Na iwapo una Roho Mtakatifu ndani yako, basi wewe una heshima ya kushirikiana na ulimwengu usioonekana pamoja na mambo ya Kimbinguni. Si ajabu watu hawawezi kuamini mambo hayo, wao hawajapata kuwasiliana. Hawana kitu *hapa* ndani cha kuaminia. Bali wakati Roho Mtakatifu anapoingia moyoni, upesi anakuwa basi m—mtu maradufu: mmoja wa duniani, wa kufa; na mwingine wa Mbinguni, wa kuishi. Amina. Katika mwili wake, yeye bado yuko chini ya mauti; bali katika nafsi yake, amepita mautini kuingia Uzimani. Katika mwili wake, yeye anawasiliana na dunia katika hisi zake tano; katika roho yake, yeye anawasiliana na Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Na Malaika wa Mungu huwazuru, wanazungumza nao, nao ni Wajumbe waliotumwa kutoka kwa Mungu kufunua, na kuleta jumbe kutoka kwa Mungu hata kwa huyo mtu binafsi. Yeye ametoka apate kupata mambo ya kwanza kwanza. Huwezi kuweka zege kabla msingi haujawekwa. Mnaona? Kwa hiyo inatubidi kukumbuka jambo hilo, kuweka mambo ya kwanza

kwanza! "Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake; mambo haya mengine yote mtapewa."

. . . Malaika akatumwa kushuhudia mambo haya . . .

56 Danieli, alipokuwa akimaliza huduma yake, nabii mkuu, kulikuweko na Malaika aliyemfuata. Ndipo huyo Malaika akamwambia Danieli, kasema, "Wewe umependwa mbele za Mungu." Na, sasa, Danieli asingaliweza kunena, labda, uso kwa uso na Mungu, lakini Mungu alimtuma Malaika kama mpa-. . . mpatanishi kati yake na Mungu, ili kwamba apate kunena kati yao, na kuleta . . . *Malaika*, neno lenyewe *malaika* linamaanisha "mjumbe."

57 Kama mvulana alikuwa mlangoni, akabisha mlango pale na kumwambia bawabu, "Nina simu hapa ya Bibi *Fulani* na Bwana *Fulani*." Yeye angekuwa mjumbe, ama malaika wa duniani.

58 Mchungaji wenu, wakati anaposimama hapa jukwaani, akihudumu Neno la Mungu, yeye ni malaika wa Mungu kwa kanisa, mjumbe kwa kanisa. Kwa hiyo mchungaji kamwe asiliache Neno hilo, bali akae moja kwa moja na Neno, kwa maana Yeye anawalisha, mahali pa mchungaji. Sababu, neno *mchungaji* linamaanisha "mchunga kondoo." Lichunguze uone kama hilo si kweli. Mchungaji ni mchunga kondoo, Naye Roho Mtakatifu alimfanya mwanglizi wa kundi fulani, kuwalisha (kitu gani?) Neno la Mungu. Amina. Loo, jamani! Ni ninii . . .

59 Angalia majina hayo yote, yanamaanisha jambo fulani, kila jina katika Biblia. Unapoona jina moja katika Biblia, linamaanisha jambo fulani. Mlijua, wake za Israeli, walipowazaa wale wazee wetu kumi na wawili . . . Kila mmoja wa mama hao, walipokuwa wanamzaa mwana, naye mwana alikuwa anazaliwa, nao wanaugua; kuugua walikosikika, na kuwapa wavulana hao majina. Na kuugua kwenyewe walikougua, kunashuhudia tabia ya huyo mwana na mahali watakapopumzika mwishoni. Kila kuugua, amina, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu!

60 Hiyo ndiyo sababu inatupasa kuwa tukiugua katika Roho. Sasa, hilo halimaanishi mengi ya maigizo haya, lakini ninamaanisha kuugua kweli kwa ajili ya Kanisa. Halafu Roho Mtakatifu . . . Ndipo unapoweza kupata kunena halisi kwa lugha na kutafsiri. "Roho Mtakatifu akikujalia kutamka, ambako kunaonekana katika kuugua na maombi," kuwa kweli kabisa, pia. Itakuwa ni kitu sasa hivi, utakachoona kikitukia.

61 Ndipo Danieli, alipokuwa akimalizia, mwishoni, aliona, "Malaika akishuka, akaweka mguu mmoja juu ya nchi na mwingine juu ya bahari, upinde wa mvua juu ya kichwa Chake. Akainua mikono yake, akaapa kwa Yeye aliye hai milele na milele, ya kwamba, 'Hapatakuwa na wakati tena,'" katika kumalizika kwa wakati ule ambao alimwambia. Kwa maneno mengine ni hivi, kipindi cha wakati wote ule ambao tunaishi

sasa, kutoka wakati huo na kule kuja kwa yule Mtawala, hata siku hii. Kisha akasema, “Katika wakati huo, siri ya Mungu itatimizwa.”

62 Na ulimwengu unaugua, ukingojea siku ya leo. Watu hawaijui siri ya Mungu. Kwa nini? Wao hawajafunzwa siri ya Mungu. Jambo ambalo wao wamefundishwa tu, “Jiunge na kanisa, weka jina lako kwenye kitabu, kuwa mtu mzuri, mfanyie mema jirani yako.” Hilo ni sawa, bali huna budi kujua siri ya Mungu! Hakuna mtu anayeweza kukufunulia hiyo ila Yeye aliyekuwa na kile Kitabu. Nayo Biblia ilisema, “Hakuna mtu awezaye kumwita Yesu ‘Kristo,’ ila kwa Roho Mtakatifu.” Hili Kanisa tukufu la kale la Roho Mtakatifu litakuja kunawiri moja ya siku hizi jinsi ambavyo hujapata kuona!

63 Na gazeti hili mashuhuri la kiinjilisti ambamo askofu wakuu na kila kitu huandika, mwandishi mkuu, Mackay, mmoja wa walio mashuhuri sana ulimwenguni kote, anayejulikana. Nakala muhimu sana kwenye gazeti lake mwezi huu, ilisema, “Kama kanisa la Katoliki ama Kiprotestanti litawahi kumpata Mungu, litaketi kwenye miguu ya pentekoste na kujifunza jambo hilo.” Amina. Mungu hajulikani kwa theolojia! Yeye hujulikana kwa Kuzaliwa upya, kuzaliwa mara ya pili. Kanisa la Kipentekoste limekubali na kuamini, nalo halijali ni nani atakayewazia lo lote juu yake. Wao wamelikubali. Sasa Ibilisi ameweka viigizo fulani mle ndani, kutupa takataka upande mmoja. Nalo kanisa la Kiinjilisti linaelekeza kwenye hizo takataka, na kuelekeza juu ya Kanisa halisi na la kweli la kipentekoste, lililozaliwa mara ya pili, likiwa na ishara zote na maajabu. Wao wako pale, bali Ibilisi ana viigizo vyake, ambavyo Biblia ilisema angekuwa navyo.

64 Lakini, kumbukeni, Danieli aliambiwa na yule Malaika. Danieli alisikia zile ngurumo saba. Zilitoa sauti zao. Danieli akanyakua karamu yake akaanza kuandika, ndipo Malaika akasema, “Usiandike hilo!” Amina.

65 Mko tayari? Hebu tuingilie jambo hilo kwa kama dakika tatu zinazofuata. Sivyo? Sikilizeni.

66 “Usiandike!” Yohana aliona jambo lile lile, na tayari lilikuwa limeandikwa upande wa nje wa Biblia; na kulikuwa na Muhuri saba nyuma ya kile Kitabu, ambapo hapana mtu angaliweza kuzifungua Muhuri hizo, hizo zilikuwa hizo sauti. Hii hapa Biblia, imeandikwa, ambayo ni siri, Yenyewe. Bali upande wa nyuma wa Biblia, zile funuo kama zilivyoonyeshwa Danieli, zinasema kuna sauti saba zitakazotamkwa, ambazo hapana mtu angaliweza kuzifunua, hakuna mtu anayejua zilikuwa ni nini. Bali Biblia ilisema, na Danieli na Yohana waliambiwa, ya kwamba, “Katika siku za mwisho, sauti hizi saba zingejulikana na Kanisa halisi na la kweli.” Mnalipata jambo hilo? Unaweza kuona mahali ambapo ule uongo na

kuigiza kunajaribu kuwezavyo kuwaweka watu mashuhiri mbali na mahali kama hapo?

67 Kabla tu ya jana, alasiri, mmoja wa watu mashuhuri sana wa kiinjilisti duniani, aliketi kwenye chumba changu, akilia, kisha akampokea Roho Mtakatifu; wanafanya mipango pamoja na Billy Graham kuja nyumbani mwangu mara atakapokuja Louisville, nina jina lake na kadhalika hapa, kuja kutafuta na kuzungumza juu ya Roho Mtakatifu, na nguvu Zake. Sasa, si kwa kunukuu jambo hili. Billy alisema, alisema mahali fulani, "Mwanamke amesimama, akilia, huku ana tezi kubwa," akasema. Ndipo kitu fulani kikamgusa, naye akaenda mbele mbio kumwombea. Naye akasema, "Nimepatwa na nini?" Loo, jamani!

68 Mungu, katika siku za mwisho, ataivuta mioyo ya kweli kutoka kila mahali. Haidhuru Ibilisi ana maigizo mangapi na makapi mangapi, Mungu ataliinua Kanisa Lake moja kwa moja kutoka mle. Itakuwa ni kule kutiwa muhuri, hakika kama ninavyosimama kwenye jukwaa hili. Nayo ile saa imekaribia. Lile baridi na la kawaida linaacha ziwa. Lile la kiinjilisti na la Injili ya umma, na mambo hayo mengine yote, yamekwisha. Ule upande wa mazingaombwe unaelekea kwenye ushupavu asili wa dini sana hata mtu ye yote aliye kipofu angeweza kuona jambo hilo. Bali Mungu analivuta Kanisa Lake litoke!

69 Kama lile nyinyoro kuu la majini. Ile mbegu ndogo, ndogo sana, iliyozaliwa kule chini kabisa katika kidimbwi cha matope, kinyaa, uchafu, koga za vyura. Nalo hujisokota likapitia gizani, kupitia matope yote na koga zote. Nalo linakuwa kitu chenye kuangaza sana ulichowahi kuona uso wake, lenye kunawiri kama jua.

70 Vivyo hivyo Kanisa la Mungu aliye hai pia, ambalo limezaliwa kule chini katikati ya ushupavu wa dini na machafuko. Bali litajisokota kupitia kwenye taka mpaka liko juu ya kitu hicho sasa, likitandaza mabawa yake lipate kuruka. "Wengi wataenda mbio huko na huko; na watu wamjuao Mungu wao watakuwa hodari katika siku hiyo." Ufunuo wa Mungu kwa Kanisa Lake! Ketini kimya, enyi Kundi dogo, kaeni mahali penu. Kama vile Dada Gertie na Dada Angie walivyozoea kuimba hapa. "Endelea kushikilia!" Usijali. Mungu anangojea, na kujaribu, na kukazana kufikia kwenye siri ya Mungu iliyofunuliwa Kanisa Lake. Jambo hilo ndilo linalozuia kule Kuja kwa Kristo sasa, na ule Utawala wa Miaka Elfu, ni hizi nguvu kuu za kimbinguni ambazo kweli hazitumiwi katika Kanisa.

71 Watu wengi wanaosimama mimbarani asubuhi ya leo, wakihubiri Injili ya Umma, lakini kule chini moyoni mwake yeye kweli anaamini. Na, ndugu, ana nguvu za kulihubiri Hilo. Anachotaka kuona, ni kulitia katika nguvu Yake, katika uzuri

Wake. Ninashukuru sana kuona jambo hilo likitimia! Nafurahi sana kuliona likidhihirishwa, Ufunuo wa Yesu Kristo!

72 "Yesu," Biblia ilisema, "ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mungu, katika rehema yake isiyo na mwisho. Kwa Neno Lake, si kitu fulani cha kisiri cha kitu ambacho ni cha ushupavu wa dini. Lakini katika kuhubiriwa kwa Neno, Yeye anajidhihirisha Mwenyewe, Bwana Yesu Kristo aliyefufuka, aliye hai. Akifanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, Yeye anayafanya tena katika nguvu Zake na kudhihirishwa. "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta watu wote Kwangu," watu wenye njaa ya moyo, watu wakuu.

73 Ule mkutano mkuu wa halmashauri, si muda mrefu uliopita, 1958. . .Niliombwa jana kuwakilisha kutenda kwa Mungu kwa kimbinguni mbele ya wajumbe mia sita na kitu kutoka kote ulimwenguni, Mungu akikawia hata mwaka wa 1958, utakuwa kule Boston, Massacussets. Mmoja wa wahudumu, mtu mashuhuri wa Injili ya kawaida, David Duplessis, alisema, "Ndugu Branham, wakati wajumbe wote wa duniani wamekusanyika pamoja na mataifa ya Kikristo yamekusanyika pamoja kutoka kila mahali kwenye baraza hili kubwa la ulimwengu," kasema, "wakizungumza tu juu ya Neno, na nguvu za kumfunua Roho Mtakatifu zikiwemo," akasema, "wale wa kiinjilisti kutoka kila mahali wataingia."

Nao wakishapata ladha yake, na Injili halisi, jambo hilo litamalizia majira ya Mataifa na kuleta kule Kuja kwa mara ya pili kwa Bwana Yesu. Mungu hawezi kuwa wa haki na kuachia mioyo miaminifu ikae kule nje na kuchachatika jehanum kwa ajili ya jambo hilo. Hana budi kuwa mwenye haki, Naye hana budi kuwapelekea hiyo, kwa namna fulani. Tuko katika siku ya mwisho.

> *Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo. . .hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika. . .*

74 Malaika! Yeye atautumaje? Mungu alimpa mtumishi fulani, nabii, Ufunuo wa Yesu Kristo, katika kisiwa cha Patmo. "Akatuma kwa mkono wa malaika." Amina. Natumaini mnaona jambo hilo. Je! Yeye si ni wa ajabu?

75 Angalia kile alichokuwa Yohana. Hebu tusome aya nyingine, nasi tutafunga.

> *Aliyeshuhudia Neno la Mungu,. . .*

76 Hakuwa ameshikwa na hamaki fulani, hakuwa ameketi kule nyuma akiwa na Injili ya umma. Yeye alidumu moja kwa moja na Neno. Yeye alishuhudia! Inawezekanaje ile. . . kushuhuhudia isipokuwa Neno lidhihirishe yale anayohubiri, kama Neno ni mbegu? Nayo mbegu itazaa! Ninawezaje kusema kuna shamba la mahindi pale, isipokuwa mbegu izae mahindi

kweli? Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu alikuwa akishuhudia kupitia kwa Yohana, ya kwamba alikuwa anahubiri Neno la Mungu.

> *. . . aliyeshuhudia Neno . . . ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo . . . aliyoyaona.*
>
> *Heri asomaye . . .*

77 Ni wangapi wanaotaka baraka? Basi yasomeni! Je! hilo si ni zuri sana?

> *Heri asomaye na wao wayasikiao* neno *ya unabii huu, kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.*

78 Loo, jamani, laiti tungaliliingilia sasa hivi! Angalieni! Ni lini ambapo wakati umekaribia? Wakati ufunuo wa Yesu Kristo umefunuliwa kwa Mwili wa Kristo. Naye Kristo amefunuliwa, hajakufa, bali yu hai, akiishi katika Kanisa Lake, akifanya mambo yale yale aliyofanya, huduma ile ile, Injili ile ile, ishara ile ile, Kristo aliyefufuliwa. Wakati amefunuliwa na Malaika Wake, kwa Kanisa, basi wakati umekaribia. Na hapajakuwa na wakati, tangu wakati huo mpaka huu, ambapo siri ya Yesu Kristo imepata kufunuliwa mpaka miaka hii michache iliyokwisha. Basi, wakati u karibu!

79 Angalia ulimwengu katika hali yake ya asili. Mabomu ya atomiki, ya haidrojeni, ya kobalti, mabomu yote na kadhalika waliyo nayo; ulimwengu mzima unatetemeka. Kila kitu, kinatikisika na kutetemeka. Viumbe vyote vinaugua. Mnajua jambo hilo. Ninalijua. Hiyo Pentagon inajua. Urusi inajua. Uingereza inajua. Ulimwengu unajua. Wakati umekaribia! Nini kinafanya maumbile kutetemeka jinsi yanavyotetemeka? Kwa sababu wakati umekaribia!

80 Kanisa hili ni, katika kukombolewa Kwake, ni mfano mkamilifu wa Israeli katika ukombozi wao, wakati Israeli ilipochukua msimamo wake juu ya Neno la Mungu lililo takatifu, lisiloghoshiwa. Ilikuwa ikitaka kusimama na kuanza kupiga hatua. Musa aliwaongoza wana wa Israeli; akiwa na mkate kidogo, mkate uliookewa juu ya kichwa chao, Kosha; nao wakapitia kwenye Bahari ya Shamu. Njia ya Mungu iliwaongoza moja kwa moja kwenye Bahari ya Shamu. "Vema," yeye akasema, "sasa tutavukaje?"

81 Basi mtu fulani akaangalia nyuma, na akasema, "Angalieni, wanakuja kule ng'ambo, vumbi linatimka. Kuna maelfu mara elfu ya magari ya Farao moja kwa moja nyuma yetu!" Hilo kundi lililochangamana lililoambatana nao, lilianza kutikisika na kutetemeka, lililofuata, hatimaye likaangamia katika maasi ya Kora. Hapana shaka bali hata asili yenyewe ya vilima ilitikisika, yalikuwa yataona moja ya mauaji mabaya sana ya kinyama uliyopata kuona. Maskini kundi dogo la watu wadhaifu limesimama pale karibu na bahari. Watoto wadogo

wakiwakimbilia mama zao, na kushika nguo zao. Maskini baba mzee akijiegemeza kwa mvulana wao, analia, akisema, "Mwanangu, nimeishi nikamaliza siku zangu, bali nachukia kukuona ukiaga dunia. Angalia, wale kule wanakuja!" Viumbe vyote vinavyoogopa mauti, hata maua, miti, na kila kitu kinginecho, kinaogopa mauti. Maumbile yalitikisika na kuugua, na kutetemeka chini ya miguu yao, yalipoona mauaji ya kinyama yakija.

82 Mungu alikuwa anafanya nini? Lakini, loo, ni kushikilia kwa jinsi gani! Wao walikosa kutambua, kulikuweko na Nguvu za kimbinguni zilizokuwa zinaning'inia kule, ile Duara ya Nuru ya Mungu, Nguzo ya Moto ikining'inia kule, ambayo ingesimama kati yao na adui huyo wakati wa kusimama utakapowadia.

83 Maumbile yakitikisika, bahari ikaanza kushikwa na wasiwasi, mwezi ukitazama chini, ukitikisika, ndege wakaondoka mahali hapo, wanyama wakatoroka. "Loo, ni mauaji ya namna gani yasiyo na mwisho! Na hao milioni ya watu watakufa katika dakika chache." Nao wote walikuwa wanaugua.

84 Bali wao walikuwa wanafanya nini? Walikuwa wanaifuata njia ya Mungu. Ilionekana ni ya kijinga, ilionekana ni wenda wazimu, bali wao walikuwa wakitembea Nuruni. Amina. Loo! Wakitembea Nuruni! Mnakumbuka tulipokuwa tunaimba huo wimbo?

Tutatembea Nuruni, ile Nuru nzuri,
Huja ambapo matone ya rehema yanang'aa;
Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

85 Yeye alifufuka katika wafu. Yuko mbele yetu. Ameonyesha ishara na maajabu, bila kukosea, si upuuzi wa ushupavu wa dini; bali ni ishara ajabu za Biblia, ya kwamba Yeye yu pamoja nasi na anatuongoza. Nasi tunaelekea mahali fulani.

86 Na kule mabomu yananing'inia, kule mabomu ya kobalti yananing'inia. Loo, jamani! Na tangazo likitangazwa sasa kukomesha wote wasio wa madhehebu, na kuungana katika kanisa moja kubwa mno la kiinjilisti la Kiprotestanti, litakaloshirikiana na kuungana na Ukatoliki, wapate kuukabili ukomunisti. Ni kazi ya Ibilisi. Naam, bwana! Mungu kamwe hakupata kushirikisha taifa na Kanisa—Kanisa pamoja. Mungu huliongoza Kanisa Lake, Naye hawatarajii viongozi wa kisiasa wawaongoze, si hata siasa za kanisa. Kila mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu yuko huru. Amina.

87 Huyu hapa, moja kwa moja hapa mwishoni sasa. Watu wakaanza kuangalia kila mahali, "Vema, tufanyeje? Tufanyeje?" Loo, ni upuuzi jinsi gani kusema, "Tufanyeje?" Mwangalie tu Yeye anayeongoza. Amina.

88 Tutafanya nini? Ndugu, nyinyi mlio na umri wa zaidi ya miaka thelathini. Dada, wewe ambaye una mvi, na baba anayeketi karibu nawe. Ninyi mlio wagonjwa na mnaoteseka. Unaweza kuuangalia mkono wako. Kila mnapoangaliana, mnajua jambo moja ni la hakika, hamna budi kufa. Kila unaposikia gari la kuchukulia wagonjwa likishuka barabarani, linasema, "Mauti yako moja kwa moja mbele yako." Kila wakati unapopita karibu na uwanja wa makaburi na kuona kaburi, linasema, "Mauti yako bele yako." Kila unapoona kunyanzi likija usoni mwako, ama nywele za kijivu, ama bega lililoinama, linasema, "Mauti yako mbele yako." Loo, bali jinsi Mkristo anavyoweza kusimama mwenye furaha, moja kwa moja ukingoni mwa Bahari Nyekundu!

89 Musa aligeuza uso wake kwa Mungu akaanza kuomba! Hiyo Nguzo ya Moto ikashuka, ikasimama kati yao na ile hatari. Giza kwao; kama ukiikataa Nuru, itageuka iwe giza kila wakati. Na ilikuwa ni giza kwao; bali ilikuwa amri ya kusonga mbele kwa hawa wapate kuendelea. Nao walipofika baharini, bahari ikafunguka. Upepo mkali wa mashariki ukija kutoka pande zote walizokuwa, ukivuma juu ya vichwa vya Farao, ukashuka na kuisukuma bahari nyuma. Nayo bahari ikaogopa kwa maana Mungu alikuwa ameamrisha njia kupita kwenye kitu hicho. Mungu alikuwa akionyesha upendo Wake kwa watoto Wake. Yeye hupenda kukuweka katika mahali pa hatari wakati mwingine, ili apate tu kujidhihirisha Mwenyewe.

Kama vile mchungaji alivyosema wakati mmoja, yeye "alivunja mguu wa kondoo."

Kasema, "Kwa nini kufanya hivyo?"

90 Kasema, "Ili nipate kumlisha, kumpenda, na kumthibitishia ya kwamba nampenda." Haya basi. Kasema, "Ndipo atanifuata."

> . . .*mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako; naye*. . .kutuma *kwa mkono wa*. . .

> *Yohana, kwa makanisa saba yaliyoko Asia: Neema na iwe kwenu na* mwongezewe *amani,* (loo, jamani), *zitokazo kwake yeye aliyeko*. . .*aliyekuwako na atakayekuja;*. . .

91 Yesu! Angalia, mambo matatu. "Aliyekuwako, aliyeko, atakayekuja; yeye ule jana, leo, na hata milele." Baadaye kidogo, katika Maandiko, sura inayofuata, Yeye alisema. . . Kutoka kwenye sura iyo hiyo, Yeye alisema:

> *Na aliye*. . .*nalikuwa nimekufa,*. . .na *ni hai* tena *hata milele na milele.*. . .*ninazo funguo!*. . .

Si kanisa fulani, Petro ama kanisa lake kuu kule Rumi, wala Jamii ya Maaskofu, ama cho chote kile, kina ufunguo. Huo ni ufunguo wa ushirika.

. . . lakini *ninazo funguo za mauti na kuzimu*. Amina.

92 Loo, hivi hamumpendi leo? Yeye ana funguo za shangwe yenu, Yeye ana funguo za furaha yenu, ana funguo za ukombozi wenu kutoka kaburini. "Ninazo funguo za mauti na za kuzimu, Jehanum. Ninaweza kufungua ya kimbinguni; ninaweza kufungua za maumbile. Ninazo funguo za mauti na za kuzimu hapa mkononi Mwangu." Loo! "Kuna chemchemi iliyofunguliwa. Njoni, nyweni maji ya Uzima, bure."

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu
Iliyotoka kwenye vena ya Imanueli,
Wenye dhambi wanapotumbukia chini ya hayo
 mafuriko
Wanapoteza waa lao la dhambi.

93 Unaporudi kutoka Kule, ndugu, haikubidi kuchukua neno la rabi, la kasisi, wala la mhubiri. Moyoni mwako kuna kitu kilichoufanya ushirika uwe mtamu, kuna kitu kilichoyafanya mambo yote ya kale kupita, na mambo hapo yakawa mapya. Kuna kitu fulani kilichokupenda kule, na kitu kilichoko moyoni mwako. Paulo alisema, "Hakuna yaliyopo, hakuna cha yatakayokuwapo, wala magonjwa, wala hatari, hakuna kinachoweza kututenga kamwe na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu." Hakuna kusengenya, hakuna hali, wala shari, hakuna kitu kingine, hakuna kitu kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu. Magonjwa, huzuni, njaa, ugomvi, tofauti kanisani, tofauti za maoni, hata iwe ni kitu gani, hakuna kinachoweza kukutenga na upendo wa Mungu.

94 Hivi hutaki kujitumbukiza leo, tunapoomba? Huyu dada, waweza kuja hapa kwa muda kidogo tu tunapoinamisha vichwa vyetu katika maombi. Kabla tu hatujaomba, sijui kama mtu fulani kanisani, kundi hili dogo asubuhi ya leo, lingesema, "Ndugu Branham, nikumbuke. Ninainua mkono wangu."

95 Nasikitika ilinibidi kufupisha Ujumbe, asubuhi ya leo, jinsi nilivyofanya. Lakini ninazo tu dakika chache, maana sina budi kuwa mahali pengine hivi punde. Na kuna ibada nyingine inayokuja, sina budi kuondoka mara moja. Nami ninataka kuwaombea wagonjwa kabla sijaondoka.

96 Lakini mnapokuwa hapa tu, je, mmeshawishika? Kweli mmepita kutoka mautini kuingia Uzimani? Hivi kweli jina lako limekuwa, ninakusudia kusema, kweli limekumbukwa? Liko kwenye Kitabu cha Mungu leo? Na, lo, wewe uko na amani na Mungu? Na ulimwengu na mambo yote ya kale yamepita, na kila kitu kimekuwa kipya? Je! kuna kitu fulani halisi, kiaminifu, kitamu sana cha kindugu na cha kitauwa moyoni mwako, ambacho unajua ya kwamba hakitolewi na ulimwengu?

Je! unawapenda wenye dhambi vizuri sana hata unapozungumza nao unakuwa tu mmoja wao? Paulo alisema angetoa maisha yake, angekuwa mtu wa kukataliwa, kama

Mungu angewaokoa baadhi ya marafiki zake wenye dhambi; kwa maneno mengine, watu wake, Wayahudi waliokuwa wanampinga. Je! hiyo ndiyo namna ya dini uliyo nayo asubuhi ya leo, ewe rafiki?

Kama siyo, kuna Chemchemi. Yote imejazwa Damu, iliyotolewa kwenye vena ya Imanueli. Kwa imani, jinsi tu unavyoweza kufanya jambo hilo, pale wenye dhambi hutumbukiza nafsi zao moja kwa moja chini ya hiyo gharika. Ni kazi ya Mungu. [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] Nini kilichotukia? Unapoteza mawaa yote ya dhambi zako. Yanaachwa nyuma yako, kama vile jeshi la Farao lilivyoachwa nyuma ya Israeli.

97 Fuata mawaidha, si miamsho; mawaidha. Kama Musa angalifuata miamsho ya watu, wangekuwa wakikimbia kote milimani, wakipiga mayowe, nalo jeshi la Farao lingaliwapata. Bali wao waliyafuata mawaidha. Mungu alisema, "Simameni kimya mwone utukufu wa Mungu. Simameni tu kimya. Haiwabidi kuichochea. Simameni kimya muone utukufu wa Mungu. Kwa kuwa, siku hii Mungu atapiga vita, nanyi mtasimama kimya." Wao walitembea wakavuka bahari. Ndipo waisotahiriwa, hao waigizaji, wakijaribu kufanya jambo hilo, walizama baharini.

98 Baba, Mungu, kundi hili dogo, dogo sana hapa asubuhi ya leo, bali kuna wanaume halisi na wanawake wanaoketi hapa walio watoto Wako, wanaokuamini Wewe na kukupenda. Naomba, Mungu, kwa ajili yao. Labda wengine wao hawajakupokea bado, bado hawajakuwa na tukio kweli la kufa kwa mambo yote ya kimwili ya ulimwengu, wao wanaishi tu kwa maungamo ya kanisa, waliwaambia watu na kuwaambia wengine. Labda wemekwisha kubatizwa ama cho chote kile, katika—katika utaratibu wa Kikristo, bali kweli hawajapata kuokolewa kweli. Wao kweli hawajui ni kitu gani. Labda wamekuwa tu na mwamsho wa kiakili, wakiungama Ukristo kielimu, wakifikiria ya kwamba wao ni sawa; kwa seminari, ambapo, "Kuna njia inayoonekana sawa kwa mwanadamu," inaonekana kama kwamba ni sawa nawe unaipata Hiyo, "bali mwisho wake ni njia za mauti."

99 Mungu, jalia kila mwanamume na mwanamke, mvulana ama msichana, wachunguze mioyo yao wakati huu; sio wao, bali hebu Roho Mtakatifu awachunguze. Na iwapo wataamua katika moyo wao, "Naam, ninaamini nimekuwa makosani. Kweli sijafikia mahali pale bado, ambapo mambo yote hayo yamepita. Ndipo nita-. . .Nami, Baba, ninakukubali sasa hivi, kuwa msaada wangu, wakati unapobisha moyoni mwangu. Bado unaniita mimi, la sivyo usingekuwa ukinena nami namna hii."

Naomba wao wainue mikono yao, si kwangu mimi; bali Kwako. Na kwa kufanya hivyo, waseme, "Tangu siku hii

na kuendelea, Bwana, ninajipeleka mpaka kwenye mto wa kujikana binafsi. Ninajipeleka kwenye mto wa mauti. Huko ninajitumbukiza kule ndani, nipate kupoteza kila waa la ubaya wangu; tabia zangu zote, na uchafu, na mawazo yangu, tofauti zangu zote, ugomvi wangu, na ubishi, na hamaki, na—na mambo hayo yote. Nitayatumbukiza tu moja kwa moja chini ya mafuriko, ili kwamba, nitakapotokea, ninataka kujisikia kama ilivyosema Injili kwamba yanipasa kuwa: msafi, tayari, nikiwa na moyo mweupe, nikiwa na upendo halisi kwa wenzangu. Hata wawe wakatili namna gani, ningali ninawapenda. Ninataka kuingia katika ushirika pamoja Nawe, mpaka nitakapojisikia kwa maadui wangu jinsi unavyojisikia; kutaka kujua kweli jambo hilo, Bwana."

Kwa kuwa, hatuwezi kuichezea sasa, tumechelewa mno. Huenda tukaaga dunia baada ya leo. Huenda tukaondoka baada ya dakika tano tangu sasa, hatutapata nafasi nyingine. Pia, Mungu, jalia wanaume na wanawake wawazie jambo hili kwa uchaji, wakiketi kwenye kanisa hili dogo leo, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo.

100 Na wakati vichwa vyenu vimeinamishwa, sijui kama kuna mmoja atakayeinua mkono wako, na kusema, "Mungu, nikumbuke mimi, mimi ndimi ninayetaka tukio hilo pamoja Nawe. Ninainua mkono wangu." Sasa, kama huna hiyo dhamana halisi na ya kweli, inua tu mkono wako. Mungu akubariki, pia. Mungu akubariki, bibi. Sasa, kila mmoja asiye na hakika unayo sasa. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, dada. Sasa jambo fulani . . . Mungu akubariki, ndugu yangu. Mungu akubariki, dada yangu . . . Wewe huna hakika kweli kweli . . . Unaona—unaona kila wakati unapopita, ndugu, tabia, yote uliyo yamebadilishwa.

"Loo, naam, ninaamini, Ndugu Branham."

101 Bali kama tu ni jambo la kielimu, unaamini kwa sababu una nia ya kuamini. Hilo silo ninalonena habari zake sasa. Ninamaanisha, kweli umeokolewa, umetiwa muhuri na upendo wa Milele wa Mungu, hata unaweza kuwapenda watu wasiopendeza kwako, na unafikia mahali ambapo unaweza kusimama mbele yao, ushike mikono yao, na si—si na washupavu wa dini, ama ushupavu wa dini, hasa, unajifanya ama hujifanyi. Uchukue mkono wake, useme, "Ndugu yangu mpendwa. Ni—ni—nimekosea. Na—naomba uniombee. Na— nakupenda." Na ukiwa na msimamo kama huo, unaweza kweli kutoka moyoni mwako kufanya jambo hilo? Unaweza?

Unaweza kuweka kando mambo yote ya ulimwengu, upate tu kumtumikia? Yeye anachukua nafasi ya kwanza maishani mwako? Kama ndivyo, ubarikiwe, na baraka Zake zitakuwa juu yako. Kama sivyo, mkubali sasa hivi Naye atakubariki, na baraka Zake ziwe juu yako. Hivi si ni afadhali awe ana

upendeleo kwako? Afadhali awe na upendeleo kwangu, na kila mtu ulimwenguni anichukie. Bila shaka, ninaamini, kama Yeye akiwa na upendeleo kwangu na kunipenda, watu watanipenda, pia; watoto Wake wote watanipenda. Naye ataniweka katika hali ambayo ninaweza kuwapenda wabaya, kama Yeye alivyofanya, maana Roho Wake angekuwa ndani yangu.

102 Mara nyingine zaidi, kabla hatujaomba. Kama kuna wo wote ambao hawajainua mikono yao, nao wanataka kukumbukwa katika maombi haya, tafadhali inua mkono wako. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu. Mungu kubariki, dada. Mungu akubariki, ndugu. Hiyo ni kweli. Sawa. Mungu akubariki, mvulana mwanangu. Sasa, Yeye anawaona. Kuna rekodi ambayo imechukuliwa asubuhi ya leo.

103 Shikeni maneno yangu. Kama mnanitambua, na, ambalo, kwa heshima mnasema jambo hilo, na kwa upendo, mnanitambua kuwa mwonaji wa Mungu. Kumbukeni, hili liko kwenye vitabu vya Mbinguni. Yeye yuko hapa. Je! usingetaka kuishi ambapo wewe unajua moyoni ya kwamba ulimwengu usioonekana uko pamoja nawe wakati wote? Kutambua, unapotoka hapa nje na kuingia kwenye gari lako, Malaika wanachukua mahali pao karibu nawe. Unapoenda kule kwenye mtu yule, mbaya kwako, ya kwamba Roho Mtakatifu anasimama moja kwa moja juu yako, huku Malaika wamekuzunguka.

“Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?”

104 Biblia ilisema hivyo. “Malaika za Bwana wanawazunguka, wanafanya kituo wakiwazunguka hao.” Hawarudi Mbinguni; wao wanafanya kituo pale. Wao wametumwa kazi za kukulinda katika safari ya maisha. Loo, si hilo ni zuri sana?

105 Sasa, Baba wa Mbinguni, wakati hautaturuhusu. Tunamsikia Roho Wako akitenda kazi ndani yetu. Nasi tunakupenda, kwa maana Roho Mtakatifu analipenda Neno. Yeye huingia katika Neno, Naye analichukua Neno na kulifunua, analifungua. Kwa maneno mengine, Yeye humfunua Yesu kupitia kwenye Neno Lake. Kwa kuwa, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, ambao ni Kristo.” Na sasa Neno linageuka moja kwa moja tena na kufunua tena, na kumdhihirisha Kristo aliyefufuka, si wa kihistoria.

106 Ee Mungu, naomba Kanisa lione jambo hilo, asubuhi ya leo. Bali ni ufunuo, Neno likilifanya Hai, Neno lenyewe likimfunua Bwana Yesu aliyefufuka. Yeye yuko katikati yetu, akingojea wakati ambapo sote tunaweza kushikana pamoja, Naye anaweza kutupeleka akatuingiza katika ule Utawala wa Miaka Elfu, tumeshinda kama mshindi katika ushindi.

107 Ee Mungu, bariki hao walioinua mikono yao. Wao wanatamani maisha hayo ya kupendeza, maisha makamilifu, yaliyowekwa wakfu, yaliyotakaswa, yaliyojazwa na Roho Mtakatifu, yaliyotolewa kwa Mungu, yakaoshwa katika Damu. Wao wanayatamani. Wanangojea sasa. Nakuomba Wewe, si kwa njia nyingine yo yote, bali jalia Roho Mtakatifu ashuke tu chini. Na watakapotoka hapa, na wapate kwamba mambo hayo yote ambayo wakati mmoja waliyashikilia yameondoka; jalia yaachwe nyuma, yamekufa. Jalia watoke, asubuhi ya leo, Wakristo wanyenyekevu, wazuri, wanaopendana na wenye imani, wakiamini. Jalia waishi huku wamejiweka wakfu sana Kwako, mwisho wa maisha yao wangekuja Kwako wakiwa na dhamana hii, ya kwamba wamepita mautini kuingia Uzimani, nao wanamjua Kristo katika Nguvu za kufufuka Kwake. Kwa sababu, si kama kwamba Yeye ni andiko tu, ama neno fulani, ama duara fulani, ama wakati fulani; bali kwamba anaishi wakati wa sasa, Yesu aliyefufuka anaishi katika maisha yao. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina Lake, na kwa utukufu Wake. Amina.

Mwizi aliyekuwa anakufa alifurahi kuona
Chemchemi hiyo katika . . . (“Na mimi je?”) . . . siku yake. (Uliifurahia?)
Na hapo nijalie, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshe dhambi zangu zote.
Nioshe dhambi zangu zote . . . (Alifanya jambo hilo lini? Labda ni sasa hivi.)
Yeye aliosha zote . . . (“Naam nilipokiri. Nikamwambia nilitamani sana jambo hilo.” Basi anaisafisha) . . . kuiondolea mbali
Nilimwambia niliitaka sana.” Ndipo anaisafisha.) . . . anaisafisha;
Na pale nijalie, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshe dhambi zangu zote.

108 Yeye si ni wa ajabu? Unajisikia msafi kweli nafsini mwako, unajisikia hukumu yote . . . Ni wangapi wanaosikia namna hiyo, wanaotaka kuinua mikono yao kwa ajili ya ushuhuda kwa mtu anayeketi karibu yako. “Dhambi zote zimeondoka. Zote ziko chini ya Damu sasa. Ninajisikia vizuri kweli juu ya jambo hilo. Nilimwamini Bwana Yesu.”

Tangu kwa imani nilipokiona kijito kile . . . (Jinsi gani?)
Kwa imani niliona kijito kile
Kilichosababishwa na jeraha Lako,
Upendo wa ukombozi ndio umekuwa wimbo wangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.

Vema, wote pamoja sasa.

Tangu kwa imani nilipokiona kijito kile
Kinachosababishwa na jeraha Lake,
. . . wa ukombozi (si *majina*, si *vitu*) . . .
umekuwa ndio wimbo wangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nife.

Na utakuwa hivyo mpaka nife,
Na utakuwa hivyo mpaka nife;
Upendo wa ukombozi umekuwa wimbo wangu
Na utakuwa hivyo mpaka ni- . . .

Pole pole, tafadhali, dada.

109 Wimbo wako utakuwa nini? "Zikiwepo lugha, zitakoma; ukiwepo unabii, utabatilika; yakiwepo maarifa, yatabatilika. Tunajua kwa sehemu, tunaona kwa sehemu, tunatabiri kwa sehemu. Bali tutakapoona, uso kwa uso, ndipo utajua kama tunavyojuliwa. Ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika; upendo mkamilifu, wa ukombozi, na usioghoshiwa wa Roho Mtakatifu, ukiingia katika nafsi ya mwanadamu aliyepita mautini akaingia Uzimani."

110 Loo, najisikia vizuri sana. Nanyi je? Ni wangapi wangetaka kuimba wimbo wa kale pamoja nami? Mngetaka kufanya hivyo? Ule tuliozoea kuimba miaka mingi iliyopita wakati hakukuweko na kitu ila vumbi la mbao kanisani. Kila mtu aliingia, akaketi chini, bila kuzungumza, kila mtu kimya tu wawezavyo kuwa, wameketi, wakitafakari. Mpiga piano angetoka. Ningekuwa katika maombi chumbani, nikisoma. Ungekuja:

Msalabani pa Mwokozi,
Hapo niliomba upozi
Akaniokoa kwa Damu
Mwana wa Mungu!

111 Mnakumbuka siku hizo? Roho Mtakatifu angeshuka katika huo unyenyekevu na upendo, anawaaminisha wenye dhambi, nao wangekuja msalabani. Hebu tuuimbe sasa, kila mmoja wetu. Ni wangapi wanaoujua? Hebu tuuimbe sasa, kwa njia ya mtindo wa kale tu sasa. Vema.

. . . pa Mwokozi
Hapo niliomba upozi;
Akaniokoa kwa Damu;
Mwana wa Mungu!

Mwana wa Mungu, wa thamani . . .
Mwana wa Mungu wa thamani!
Hapo niliomba upozi
Mwana wa Mungu!

Sijui kama mnaweza tu kuinamisha vichwa vyenu kwa muda kidogo.

Damu ya Yesu ya thamani,
Huniokoa makosani, (nawe je?)
Huniongoza wokovuni; (Loo, jamani!)
Mwana wa . . .

Sasa hebu inamisheni vichwa vyenu tu na kuomba.

Basi, Mwana wa . . .

112 Wazia jinsi amekuwa mwema kwako, majaribu mengi uliyopitia. Wakati yule mtoto mchanga alikuwa mgonjwa, Mungu alimponya. Wakati ulipokuwa umelala kule hospitalini, nusukaputi ikikungojea, nini kilitendeka? Ni nani aliyekuponya? "Mimi ndimi Bwana nikuponyaye." Kumbuka uliyosema ulipoanza kule chumbani? Kumbuka ulivyofikiri usiku ule wakati ulipokuwa na . . . ulipokuwa na mshtuko wa moyo? Ee Mungu! Yeye angefanya nini?

Mwana wa Mungu!
Mwokozi wangu!
Hapo niliomba upozi, (akakuchukua kwa neno lako)
Mwana wa Mungu!

Sasa hebu tuuvumishe. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Mwana wa Mungu*—Mh.]

113 Sasa nyosha mkono wako kwa mtu anayeketi karibu nawe, ushike mkono wake, useme, "Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Nina furaha sana mimi ni Mkristo. Nawe je? Peana mkono na mtu anayeketi karibu nawe.

Hapo niliomba upozi;
Mwana wa Mungu!

114 Na—napenda tu kujisikia namna hii. Ninapenda kumwabudu Mungu katika utulivu namna hii. Kitu kilicho na maana halisi kwake. Kujisikia tu ya kwamba Kitu Fulani kiko karibu! Nini kilitukia? Kwenye wito wa madhabahuni, wakati hao wenye dhambi walipomkubali Kristo, Malaika waliinuka kutoka kwenye viti vyao. Mnaona, hiyo ndiyo inayowafanya kujisikia namna hii. Unaamini jambo hilo, Ndugu Hickerson?

Loo, Mwana . . .

Huku ni kuabudu, wakati nafsi inapomwabudu Mungu. Neno limetolewa, mnaona. Roho Mtakatifu anabariki na kutia maji sasa.

. . . wa Mungu!
Hapo niliomba upozi;
Mwana wa Mungu!

115 Baba yetu wa Mbinguni, wakati Uwepo mzuri na mtakatifu wa Roho Mtakatifu ambaye sasa anasimama hapa akiwabariki watoto Wake, mara nyingi imembidi kuwasahihisha, "Kwa maana kila mwana anayemjia Mungu, hana budi kwanza

kurudiwa na kujaribiwa, kupokea malezi ya mtoto, marudio," hakuna asiyerudiwa; kila mmoja. Bali tunapovumilia marudio ya Baba, basi yanazaa matunda ya sasa na yaliyo matamu. Naomba, Mungu, ya kwamba utamwacha tu kila mtoto ajue jambo hilo. Si kuondoka, kuwazia tu, bali kuwaacha wajue ya kwamba hizi ni baraka Zako kwao. Maziwa ya kweli yasiyoghoshiwa ya Injili, yakitiririka kutoka nafsini mwao, maziwa na asali yanayotoka katika Nchi ya Kanaani, divai mpya kuwachangamsha katika imani; kuabudu, mioyo iliyoinamishwa mbele Zako, mikono iliyoinuliwa, machozi yakitiririka mashavuni, wakiabudu kimya, kwa uchaji.

116 Ee Mungu, nina furaha sana! Ninakupenda sana, Bwana! Ninataka kukueleza ninavyojisikia, kama nikiweza, katika shukrani tu, nikionyesha ibada halisi ya moyo, ya kwamba mimi nakusujudu Wewe sana, Wewe usiye na kifani. Nakupenda. Mara nyingi, katika majaribu makubwa, nikiona ndege ikitikisika hewani, ikianguka, ikiyumbayumba kila mahali; nami naangalia ardhini chini yangu, inazunguka-zunguka upesi; maombi madogo tu, nayo inanyosha; nikijua tungetupwa tufe katika dakika moja. Nikisimama kule mbele ya wachawi na mashetani, wakinisai na kusonga mbele; maombi madogo tu, yanawafanya wasimame, wamelemaa.

Jisi pepo wanapiga makelele na kuwatoka watoto Wako, kwa maombi. Loo, upendo Wako, Bwana! Kuona watoto, wagonjwa, wakija, wanasema, "Baba, utaniombea?" Tunakuona ukituliza hiyo homa, unamnyamazisha mtoto, kama mama akimtuliza kwenye kifua chake. Jinsi tunavyokushukuru! Labda shida inakuja. Tunajua, tunapoangalia mbele na kuona mawimbi ya dhoruba kubwa za mauti kule ng'ambo. Kama Daudi wa kale alivyosema, "Sitaogopa mabaya, Wewe upo pamoja nami." Tunakushukuru. Tunakusujudu. Tukiona watu wakikujia Wewe; vilema, wanaoteseka, na vipofu, viziwi, na mabubu wakiponywa, kama thibitisho la Uwepo Wako.

117 Bariki wasikilizaji hawa wachache tunapongoja. Tunakushukuru kwa ajili ya kila mtu aliyekujia. Na tunaomba ya kwamba utawabariki mno mno leo. Na jalia, tangu siku hii na kuendelea, shida zao zote na majaribu zitakwisha; jalia vita baina yao na Mungu vitatuliwe sasa hivi, nao wapatanishwe kwa Mungu kwa Damu ya Mwanawe, tukijua ya kwamba Yeye alimtoa Mwanawe kuchukua vita baina ya Mungu na mwanadamu, kumpatanisha mwanadamu na Mungu, ambaye alikuwa adui wa Mungu wakati mmoja, bali sasa ameletwa karibu, Naye Mungu amewapatanisha kama wanawe na binti. Sasa wao si adui tena na wageni, bali ni watoto wapendwa. Tunaomba ya kwamba utawajalia kutambua jambo hilo. Usiache aodoe hilo kutoka moyoni mwao. Bali jalia yeye, wajalie watambue ya kwamba Wewe umebisha mioyoni mwao nao wamekukubali, wakainua mikono yao. Hilo lilitosha, Bwana.

Na sasa tunaomba ya kwamba wao watatambua jambo hilo na daima wakupende na kuwapenda wenzi wao. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutatembea katika Nuru hii, Ni Nuru nzuri
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'aa;
Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Njoni, enyi watakatifu wa imani, tangazeni,
Yesu, Nuru ya ulimwengu;
Nidpo kengele za Mbiguni zitalia,
Yesu, Nuru ya . . .

Mnampenda? Hebu tuuimbe sasa, sivyo?

Tutatembea katika Nuru hii, Ni Nuru nzuri
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'aa;
Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

118 Naona nimejazwa tu kutokana na ufufuo. Loo, hebu tuuimbe tena. Sivyo? Hebu tufunge macho yetu na kuinua mikono yetu. Canada, po pote ulipotoka; kundi hili dogo la watu hapa limetoka mahali mbalimbali nchini. Hebu tuimbe sasa, tufunge tu macho yetu, tuinue mikono yetu.

Tutatembea katika Nuru hii, Ni Nuru nzuri
Inakuja ambapo matone ya umande wa rehema yanang'aa;
Angaza kutuzunguka mchana . . . (Ee Mungu!)
Ee Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Ucheze tu muda kidogo, dada.

119 Katika Agano la Kale, Yeye alikuwa Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Hiyo ilikuwa ni Kristo, Malaika wa agano. Wote wanaojua jambo hilo, waseme. "Amina." [Kusanyiko, "Amina."—Mh.]

120 Katika Agano Jipya, Yeye alijidhihirisha katika mwili, apate kuondoa dhambi, kuturudisha tuwe wana na binti za Mungu.

121 Siku moja, chini barabarani, akaja maskini Myahudi mmoja mdogo, mfidhuli, naye alikuwa anashuka kwenda kuwakamata hao watu waliokuwa wanalia na kumsifu Mungu, na kutabiri. Basi ni kitu gani kilichokutana naye? Nuru nzuri. Yesu ana Mwili gani leo? Nuru, Nguzo ile ile ya Moto aliyokuwa ndani yake hapo mwanzo. Alikutana na Sauli wa Tarso, nayo ile Nuru ikamkaribia sana, ikaingia machoni mwake, hata ikampofusha, kasema, "Mbona waniudhi Mimi?" Kasema, "U nani Wewe, Bwana?" Kasema, "Mimi ni Yesu."

122 Leo, Huyu hapa, Yeye yuko pamoja nasi. Hata tuna picha Yake. Je! Yeye ni mwema? "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Ndipo basi ati tutafanya nini?

Tutatembea katika Nuru, (Yeye hudhihirisha
Neno Lake. Yu hai.), Ni Nuru nzuri
Huja ambapo matone ya umande . . .

Sasa hebu wagonjwa waje wayazunguke madhabahu sasa, wanaotaka kuombewa.

Angaza kutuzunguka mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya . . .

Nataka uucheze, *Ni Tabibu Wa Karibu.*

123 Jambo fulani limeingia moyoni mwangu. Ninakumbuka wakati mmoja katika ibada, nilikuwa ninawaombea wagonjwa. Na kuna bibi aliyemleta jukwaani msichana kilema. Na Roho Mtakatifu alikuweko. Nao . . . Sasa, tutamaliza tu katika dakika kumi zifuatazo. Nao wakamleta msichana mdogo kilema, naye alikuwa na—na polio kidogo, wanasema iliitwa kipooza, kipooza cha watoto. Nayo miguu yake midogo ilikuwa imekunjamana, naye hangeweza kutembea. Mnajua nilikuwa na ibada hii ya kuponya wapi? Inaonekana ni jambo geni, ilikuwa kwenye mkutano wa Dunkard, Dunkard, si wa Kipentekoste; Dunkard. Hakuna mtu aliyejua nilikuwa kule, hakuna moja ya makanisa. Bwana alinielekeza tu kule. Wao hawakujua kitu juu ya ubatizo wa Roho. Nena kuhusu Mbingu duniani, upendo ulishuka kama ulivyofanya sasa. Nikasema, "Sasa, tutaanza mstari wa maombi." Nikasema, "Ninyi nyote mlio na kadi za maombi," nikianzia kwenye nambari fulani, "simameni mkono wangu wa kulia." Wao walikuwa wanapanda juu. Kama mtu wa pili, alikuwepo bibi aliyekuwa anambeba mtoto mdogo kilema, msichana mdogo. Roho Mtakatifu akaanza kunena juu yake. Ndipo yule bibi aliyeketi kwenye piano, alikuwa anacheza:

Ni tabibu wa karibu,
Tabibu wa ajabu,
Na rehema za daima,
Ni dawa Yake Yesu!

124 Wakati alipokuwa anacheza vipande hivyo vya pembe za ndovu. Nilikuwa na chupa ndogo ya mafuta mfukoni mwangu, nilikuwa nimeyatengeneza. Ilikuwa ni halzeti yaliyotoka kwenye mzeituni. Nami nikatoka nikaenda nikawaombea wagonjwa usiku huo, nikaingia katika Roho nikaanza kulia, machozi yakaanza kutiririka usoni mwangu. Nilikuwa na mafuta haya, kwa hiyo nikakuta kwamba mafuta haya yalikuwa . . . machozi yalikuwa yakiingia kwenye mafuta haya. Nikaenda nikachukua vitu vingine vitatu, maradhi . . . vitu, na kutia mafuta mle. Nikachukua nikamtia mafuta msichana huyo mdogo kwa hicho.

Nikamwekea mikono yangu. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, wewe ni Tabibu mkuu, na Wewe uko papa hapa sasa."

Ndipo huyo msichana mdogo akaangalia nilikokuwa, akajongea kidogo, akaruka kutoka kwenye mkono wangu, akaanguka sakafuni, akaenda akikimbia chini sakafuni. Mamaye akazimia; Dunkard. Naye yule bibi kwenye piano akaangalia kila mahali, ndipo akageuka akawa mweupe sana kisha akazimia. Nayo piano ikaendelea kucheza:

Ni tabibu wa karibu,
Tabibu wa ajabu,
Na rehema za daima,
Ni dawa Yake Yesu!

125 Maskini msichana mdogo wa Dunkard ameketi pale, nikamwona akipumua kwa shida sana. Yeye hakuwa amesikia habari za pentekoste. Mtoto mdogo mwenye sura nzuri, nywele ndefu nyeupe zimetengenezwa vizuri. Unajua jinsi wanavyovaa, zimefunikwa kwa hizo kofia ndogo nyeupe. Ilianguka tu kutoka kichwani mwake. Akainua mikono yake akaanza kuimba. Hakujua alichokuwa anaimba, alikuwa katika Roho.

126 Ndipo kanisa lote, kwa moyo mmoja, likaja, wakilia kwenye madhabahu na wakamkubali Bwana Yesu. Ndipo Roho Mtakatifu akawabatiza, kila mmoja, katika upendo. Jinsi wanavyolia, na kusahihisha mambo, na kupeana mikono mmoja kwa mwingine, yakitukia. Hiyo ni pentekoste.

127 Yesu yeye yule yuko hapa. Sasa usijaribu ku-. . .Mnaona, unajaribu kufikiria, "Vema," umeweka nia yako kwenye kitu kilicho kule mbali, na labda *hiki*, ama, "Nitabahatisha." Afadhali urudi kwenye kiti chako, labda uamue moyoni mwako, "Hivi ndivyo ilivyo!" Unapopata hilo, imekwisha. Mpaka wakati huo, ingali pale.

128 Sasa kama mtasogea, sogeeni karibu sana mwezavyo madhabahuni, mkajaze nafasi. Nitamwomba Ndugu Neville anisaidie. Haya hapa mafuta ya kupakwa; ninataka Ndugu Neville amtie kila mmoja ninapowawekea mikono. Sasa, kama kweli mnaamini jambo hili, imekwisha! Aminini kweli kwa moyo wako wote. Sasa hebu tuimbe polepole sana pamoja, sisi sote, tunapoimba sasa, *Ni Tabibu Wa Karibu*.

Ni tabibu wa karibu,
Tabibu wa ajabu,
Na rehema za daima,
Ni dawa Yake Yesu!

Imbeni malaika,
Sifa za Yesu Bwana,
Pweke limetukuka,
Jina Lake Yesu.

Sasa vichwa vyenu vimeinamishwa.

Enendeni na amani,
Hata Kwake . . .

129 Baba yetu wa Mbinguni, "Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule," Neno linasema. "Naye Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi." Basi, Mungu, jalia tusiwe kamwe, kamwe na hatia ya kuifanya Injili ngumu sana kwa watu hata mpaka watafikiri ilikuwa ni mwanadamu badala ya Mungu. Sasa tutafuata tu amri. Na tukiwa na nyimbo hizi na nyimbo za dini, tumeingia katika ushirika uliobarikiwa sisi kwa sisi. Kwa hiyo, tuna Kuhani Mkuu ambaye amekuja pamoja nasi, ameingia pamoja nasi, Naye anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. Wengi wanasimama madhabahuni asubuhi ya leo, wahitaji. Nami ninamtuma mtumishi wako mpendwa na mwaminifu, Ndugu yangu Neville, mtu mwaminifu, mwenye haki; kama Eliya, mwenye tabia moja na Eliya, sisi sote. Nami ninamtuma.

130 Wewe ulisema, "Na wawapake mafuta, wawaombee," *wao*, Washiriki, "kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule." Nami ninaomba kwa moyo wangu wote, Bwana, kwa kila mtu hapa. Wewe unajua haja zao. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utawaponya. Sasa, Yakobo aliandikia hayo Kanisa, chini ya kutiwa pumzi na Roho Mtakatifu aliyepewa na Mungu, aliyefanywa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia.

131 Yesu, katika kuondoka, alisema, "Wao pia wanapaswa kuweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

132 Ninapomtuma ndugu yangu kufanya kazi ambayo Yakobo aliagiza kwa njia ya Roho Mtakatifu, kupaka mafuta; tunarudi pia kwa agizo la Bwana Yesu na Roho Mtakatifu, kuwawekea mikono. Nao watapata afya.

133 Sasa, Bwana, kwa moyo wangu wote, na kuna watu wengi asubuhi ya leo wanaoungana nami, kwa nguvu zangu zote, na uwezo wangu wote, ninaomba maombi ya imani kwa ajili ya kila mtu anayesimama hapa, nikiomba ya kwamba hawatakuwa na tashwishwi yo yote moyoni mwao, bali watarudi kwenye viti vyao wakiwa katika hali ya matumaini halisi na makamilifu ya kwamba agizo la Mungu limetimizwa kwao, na Neno Lake ni hakika litadhihirishwa katika kuponywa kwao. Ninawaombea baraka hii, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

134 Sasa kila mmoja awe. . . [Mahali patupu kwenye kanda. Mpiga piano anacheza *Damu Imebubujika* na *Ni Tabibu Wa Karibu*, huku Ndugu Branham na Ndugu Neville wanawaombea wagonjwa. Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]

135 Wakati nilipomwombea msichana mdogo na kutabiri juu yake, kama kitu kikubwa kilichotokeza kwenye kichwa chake na juu ya uso wake *hapa*, jinsi kingepungua na apone. Huyu hapa huyo msichana mdogo, huku kitu hicho chote kimetoweka, juu ya uso wake na po pote pale. Mama anamleta, kwa utukufu wa Mungu, na kuonyesha kwamba chote kimekauka, hakuna kitu kilichosalia ila kigaga. Dada, Yesu alisema wakati

mmoja, "Hawakuponywa tisa?" Mmoja alikuja kumpa utukufu, mnaona. Mungu ashukuriwe kwa jambo hilo. Sasa, mpenzi, nywele zitamea juu ya hicho. Kumbuka jinsi Ndugu Branham alivyokwambia pale usiku ule, nawe utapata afya kabisa na upone.

Na tuiname tumshukuru Mungu.

136 Sasa, Baba, tunakushukuru kwa sababu ya kuponya Kwako. Na tunakushukuru kwa sababu ya huyo mama mwaminifu na msichana mdogo mzuri, waliokuwa tayari kuja na kuonyesha ya kwamba Yesu angali anaishi na kutawala. Kuona kitu hicho kama kansa kubwa, yenye sura mbaya, imevimba kila mahali kichwani mwake na upande mmoja pale, Nawe ukamponya na kuiondoa. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hilo. Nasi tunaomba sasa ya kwamba utambariki huyo mama mwaminifu, ambaye moyo wake umefurahi sana. Wakati huyo msichana mdogo amekuwa mwanamke, na awe angali anashuhudia sifa Zako.

137 Sasa naendelea kuweka mikono yangu juu ya wagonjwa, huku mimi pamoja na ndugu tukiwapaka mafuta. Naomba wapokee aina ile ile ya baraka kama msichana huyu mdogo alivyopokea. Laiti wangaliamini tu katika imani kama ya mtoto, kama huyo mtoto alivyofanya, ingetimia.

[Ndugu Branham na Ndugu Neville wanaendelea kuwaombea wagonjwa. Mahali patupu kwenye kanda.—Mh.]

138 Sawa kabisa. Nina furaha sana asubuhi hii, ya kwamba tuko katika wakati wa kuabudu na kuwa na wakati huu wa ushirika pamoja, mmoja kwa mwingine, huku Damu ya Bwana Yesu inatusafisha na dhambi zote. Nami..

139 Kwa wageni miongoni mwetu, tunataka kuwakaribisha tena. Njoni tena usiku wa leo, kwenye ibada ya jioni. Kama mko mjini na mngetaka kurudi mwe pamoja nasi tena usiku wa leo, ningefurahi sana. Milango iko wazi daima. Hatuna madhehebu, hatuna kanuni za imani . . . Kristo, hatuna sheria ila upendo, na hatuna kitabu ila Biblia. Nasi tunawataka ninyi, tunawaalika, nanyi mmekaribishwa kwa furaha.

140 Na pia ninauliza, mnapoenda safarini mwenu, mnapoondoka mjini mwetu na mahali mbalimbali nchini, mnikumbuke kwa maombi yenu, kama mtumishi mwenzenu katika Kristo, na katika—na katika upendo na ushirika wa Roho Mtakatifu. Sina budi kuondoka karibuni sana sasa, kwe—kwenda Canada, na California. Kwa kweli, ninaondoka kwenda California. Kwa hiyo basi na—nawatakeni mwe katika maombi kwa ajili yangu, mwombe sana, sasa ndio wakati nina jambo fulani sina budi kufanya maamuzi mara moja, mnaona, na linahangaisha sana, nami na—na—naomba ya kwamba mta—mtanitia moyoni mwenu na kunikumbuka. Kwa sababu, ninajua

ya kwamba maombi ndiyo yanayobadilisha mambo. Maombi ndiyo yanayotufanyia mambo.

141 Na sasa, leo, na—nasikitika kwa kuwachelewesha namna hii, na kumweka ndugu yetu mpendwa, mchungaji hapa, mbali na mimbara yake. Ninasikitika sana, bali labda tu sijui...Sina budi kuondoka upesi sana. Nami sikuona ye yote aliyetaka mazungumzo ya faraga, waliowekwa kwenye dawati. Lakini wakati mchungaji anachunguza...Ndugu fulani alitoka huko mbali Uingereza, akasema, kuniona kwa dakika chache tu. Nami nataka kumwona ndugu huyo. Laiti ningalikuwa na wakati kuwapa mkono na kuwaona ninyi nyote, bali sina. Sasa, ili upate mazungumzo ya faragha ma—madogo kwenye asubuhi hizi wakati nikiwa hapa, mpigie simu katibu, Ndugu Cox anayeketi hapa, naye hutoa mambo hayo. Hiyo ndiyo sababu hatuna—hatuna budi kupanga wakati wetu, kusudi tuweze kuyapatia nafasi. Lakini ndugu huyu, bila ya kujua jambo hili, na kwamba anatoka Uingereza. Ninapaswa kuwa nimeondoka hapa katika dakika kumi na mbili zifuatazo, kwa hiyo mimi—mimi, naam, saa sita, kwa hiyo si—sina budi kuharakisha na kuondoka. Na kwa hiyo nyote mniwie radhi, nitaingia chumbani pamoja na huyo ndugu kwa ajili ya mazungumzo ya faragha, kwa dakika chache. Nami nitawaona ninyi nyote tena mara nitakaporudi. Niombeeni.

142 Ibada sasa zitakuwa katika—katika Kanisa la Filadelfia, Alhamisi usiku. Tutakuwa kwenye Ukumbi wa Convention, juma hili lijalo, Jumatano usiku. (Asante, bwana.) Tutakuwa kwenye—kwenye—kwenye Ushirika wa Wafanyi Biashara Wakristo Wa Injili Yote, Kimataifa. Nami ninapaswa kunena kwenye usiku wa...asubuhi ya tarehe ishirini na tatu, katika Leami-...Hoteli katika—katika Minneapolis, Minnesota. Na halafu kwenye Ukumbi wa Convention, nafikiri ndio, unaofuata, usiku huo, hiyo ni Jumamosi. Na Ju—Jumapili, niko kwenye Maskani ya Heart’s Harbor pamoja na Kasisi Gordon Peterson, na hiyo ni ibada ya kuhubiri. Na Jumatatu usiku, na Jumatatu nzima, katika mkutano kwa siku tano.

143 Halafu nina BWANA ASEMA HIVI ninayopaswa kumpelekea mwanamke fulani huko mbali katika Canada ya kaskazini. Nami nitaenda kule, mke wangu ataambatana nami, na watoto, kwa muda mfupitu. Ninarudi ku—ku, kupitia hapa, kumwona rafiki yangu, Ern Baxter. Nina jambo la kumwabia huko Vancouver. Na mara baada ya jambo hilo, nitashuka niende Washington, kwa Bw. Rasmussen, kumtembelea kule kwa siku moja.

144 Ndipo nitashuka niende La Crescenta, California, kuweka mambo fulani katika utaratibu, ambapo, hema yangu tayari imetengenezwa na iko tayari kuingia kazini sasa. Na kwa hiyo, vema, labda nitaanzia kwenye Pwani ya Magharibi ya California, kupitia California na Arizona, majira haya yajayo

ya kipupwe, Bwana akipenda; isipokuwa kwa wakati ulio wazi katikakati ya mikutano kwa ajili ya ibada ya kuingia Afrika tena. David DuPlessis na wengi wa watu hao hapa kutoka Afrika, ambao wanataka kuanzisha Kampeni ya Afrika, walikuwa pamoja nami katika mkutano huu. Tutakutana kule, inatubidi kukutana na Ndugu Arganbright na kufanya maombi, tuone ni wapi mkutano unaofuata utakakokuwa.

145 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Basi hamna budi kunipenda, kama mnampenda, kwa maana mimi niko ndani Yake. Nasi tunapendana. Bwana awabariki.

Ndugu yetu Neville, Mungu akubariki. Nashukuru kwa ajili ya wakati huo, Ndugu Neville.

Ufunuo, Kitabu Cha Mifano SWA56-0617
(Revelation, Book Of Symbols)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Juni 17, 1956, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1996 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1996 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org